**UTUMISHI** yaanika wataalamu wake sugu kwa ukiukaji maadili kazini
UKURASA 2

**KAUSHA** damu inavyosababisha msongo mawazo, kukimbia makazi
UKURASA 17

**NAIBU** Rais Kenya augua ghafla, kesi yake yasitishwa
UKURASA 19



**TUCHEL AANIKA MIKAKATI YAKE ENGLAND**
UKURASA 21

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Ijumaa Oktoba 18, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581833

www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0745 700 710 nipasheTZ nipasheTZ nip... The nipashe Digital nipashedigital



### HUKU AKITUHUMIWA UONEVU...

# Kamishna Awadhi: Hatubebi chama

**WANASIASA** wamjibu "uhalisia una shida..."

UKURASA 2



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Hitoshi Ara, wakitia saini hati ya makubaliano ya mkataba wa msaada wa yen bilioni 4.07 (Sh. bilioni 68.5) kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa ndani ya Jiji la Dodoma. Hafla hiyo ilifanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Fedha, Dar es Salaam jana. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

UKURASA WA 3

## MKULIMA KUWASHTAKI VIGOGO TUHUMA KUSHUSHA BEI YA PAMBA

MKULIMA wa pamba, Thomas Nkola, mkazi wa mkoani Simiyu...

## Wachoma nyumba, wazuia Zimamoto nyumbani kwa mtuhumiwa wa mauaji

**NI** bosi dhidi ya dereva bodaboda... *Ukurasa 3*

## Teknolojia mpya TRA kuepusha maumivu walipakodi

UKURASA 3

**MICHEZO** **BACCA ASHUSHA PRESHA YANGA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

## HABARI KITAIFA

# Utumishi yaanika wataalamu sugu ukiukaji maadili kazini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI YA Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeanza kupokea tuhuma na malalamiko kuhusu kuwapo kwa viashiria vya mmomonyoko wa maadili kinyume na mila na desturi vinavyohusu vitendo vya mapenzi ya jinsia moja kwa baadhi ya watumishi wa umma.

Aidha, ofisi hiyo imepokea mrejesho kutoka kwa wananchi wanaohudumiwa kuhusu hali isiyoridhisha ya mavazi kwa watumishi wa umma.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Xavier Daudi, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye ufunguzi wa kikao kazi baina ya ofisi hiyo, taasisi zinazosimamia maadili na mamlaka zinazosimamia maadili ya kitaaluma.

Alisema vitendo hivyo ni miongoni mwa vya kijinai kwa mujibu wa sheria za nchi, na kinyume cha maadili kwa mujibu wa miongozo ya utumishi wa umma.

"Tumieni kikao kazi hiki, kujadili na kubadilishana uzoefu ili kuja na mapendekezo ya namna sahihi ya kudhibiti vitendo hivi na namna sahihi ya kushughulikia masuala haya yatakapojitokeza katika maeneo yenu ya kazi kwa baadhi ya watumishi wanaohusishwa navyo ili kuepuka kuchafua taswira ya utumishi wa umma kwa ujumla," alisema.

Pia alisema wamepokea taarifa za malalamiko mengi kutoka vyanzo mbalimbali, yatokanayo na vitendo vya ukiukwaji wa maadili ya utendaji na maadili ya kitaaluma katika utumishi wa umma yakiwahusisha baadhi ya watumishi wa kada za wauguzi, madaktari, walimu, maofisa utumishi, maofisa ardhi, wahasibu katika halmashauri, wataalamu sekta ya ugavi wa umeme na maji, pamoja na wahandisi wanaosimamia miradi ya maendeleo.

"Wajibu wa kusimamia maadili ya watumishi wa umma katika utumishi wa umma ni mtambuka ambalo kisheria liko chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mujibu wa kifungu cha 8(3)(e) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298," alisema.

Aidha, aliwataka wajumbe wa kikao hicho kupitia Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 6 wa mwaka 2020 kuhusu Mavazi kwa Watumishi wa Umma, ili kujengeana uelewa wa pamoja kupitia uzoefu watakaobadilishana. "Mtakaobadilishana uzoefu kuhusu utekelezaji wa waraka huo kwa watumishi walioko kwenye maeneo yenu, na muweze kuchukua hatua ipasavyo kwa wanaokiuka waraka husika ikizingatiwa kuwa, mwonekano wa watumishi wa umma wanapotoa huduma unabeba taswira ya taasisi, utumishi wa umma na serikali kwa ujumla," alisema.

Aliwahimiza kujenga uwezo wa watumishi kimaadili kupitia mafunzo ya maadili katika maeneo yao ya kazi na matumizi ya serikali mtandao katika utoaji wa huduma ili kudhibiti vitendo vya uvunjifu wa maadili na kufanya utafiti mbalimbali wa kubaini hali ya uadilifu katika taasisi zao.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Usimamizi wa Maadili, Ally Ngowo, alisema wanatarajia kupokea taarifa ya utendaji kazi kwa kipindi cha Septemba 2023 hadi Septemba 2024 katika maeneo yao kuhusu suala la maadili.

Alitaja mada watakayojadili kuwa ni umuhimu wa matumizi ya mfumo wa E-Mrejesho katika matumizi ya maadili ya utumishi wa umma.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, akizungumza wakati wa kongamano la jukwaa la majadiliano kuhusu masuala ya nishati kwa Bara la Afrika (AEMP) kwa ngazi ya mawaziri unaofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: OFISI YA NAIBU WAZIRI MKUU**

# Kamishna Awadhi: Hatubebi chama

**Na Pilly Kigome**

JESHI La Polisi nchini limewataka wananchi na vyama vya siasa kuacha kulinyooshea vidole kwamba linakandamiza baadhi ya vyama katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Uongozi wake umesema jeshi haliko kumlinda mtu au chama chochote kitakachovunja sheria na kuahidi kusimamia kutenda haki na si kuvunja haki.

Jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Operesheni na Mafunzo, Kamishna Awadhi Juma Haji alitoa kauli hiyo kwa niaba ya Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) wakati wa mafunzo ya siku mbili (kuanzia jana) yaliyoandaliwa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) kuwajengea uwezo makamanda wa polisi mikoa kuelekea uchaguzi ujao.

Kamishna Awadhi ametoa kauli hiyo kipindi ambacho Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kinamtuhumu kukiuka sheria za uchaguzi, pia yeye binafsi kuwapiga baadhi ya viongozi wa chama hicho, wakiwamo Makamu Mwenyekiti Tundu Lissu na Katibu Mkuu John Mnyika. Kuna kusudio la chama hicho kumfungulia mashtaka mahakamani.

Aliwaomba Watanzania kuondoa dhana hiyo aliyoiita "potofu" kwa kuwa jeshi lipo kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa raia na kumwajibisha yeyote atakayekiuka sheria bila kujali ukubwa wa chama anachotoka.

"Hatupendelei mtu yeyote wala chama chochote kile, tuko katika majukumu mazito ya kusimamia sheria, hivyo kwa yeyote atakayekiuka sheria, basi tutawajibika, haijalishi ni nani," alisema.

Kamishna Awadhi alisema mafunzo hayo yamewakumbusha majukumu yao kwa kuwakumbusha kutoingilia kazi za watu wengine kama mahakama na taasisi zingine ambazo wanashabihiana katika utendaji kazi.

"Wajibu wetu mkubwa ni kuhakikisha tunadumisha amani katika kipindi hiki cha uchaguzi, kudumisha amani na haki ili Tanzania iendelee kuwa kinara wa amani katika demokrasia duniani kote," alisema.

Mratibu Kitaifa wa THRDC, Onesmo Olengurumwa alisema wamewaleta pamoja makamanda hao ili kuwakumbusha kazi zao kuelekea uchaguzi kwa kusimamia sheria za uchaguzi.

"Pia kuwakumbusha maadili, miiko, misingi ya haki za binadamu wakati wa uchaguzi, mambo ya msingi wakati wa uchaguzi, uhuru wa kuongea, mbinu ambazo ni salama kutumia kulinda na kuleta amani wakati wa uchaguz," alisema.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, aliambia Nipashe jana kuwa wana imani na polisi, lakini watawapima zaidi kwa matendo yao kuliko maneno huku akiwataka kuacha kujivika alichodai "u-CCM" wanapotekeleza majukumu.

"Tutawahukumu kwa matendo yao, tuna malalamiko mengi kwamba polisi wanasisima na CCM, hawatendi haki, wanawalinda watu wa CCM, tutawahukumu kutokana na matendo yao, popote watakapokwenda kinyume cha haki tutawasema," alisema.

Dorothy alisema ili anachokisema Kamishna Awadhi kiaminike, ni vyema wakaacha kuegemea chama kimoja, akitolea mfano wanavyozuiwa kufanya mikutano ya hadhara na baadhi ya viongozi kukamatwa saa chache kabla ya mkutano.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema jana kuwa hakuna dhana kuwa polisi wanabeba chama kimoja bali kuna ushahidi wa wazi.

"Mpaka leo kijana wa CCM aliyemjeruhi kiongozi wetu kituoni Kata ya Tabata, Kituo cha Mtaa wa Msimbazi hajafikishwa mahakamani pamoja na kumjeruhi vibaya kwa kiwembe, jambo ambalo lingeweza kusababisha kupoteza maisha.

"Tukio la pili lilitokea huko Ukonga, kijana wa CCM amemjeruhi vibaya kiongozi wa CHADEMA kwa kumpiga na jiwe. OCD wa Mpanda alizuia mikutano ya hadhara ya CHADEMA na kusema muda wa kampeni bado, ila vyama vingine vinaendelea na mikutano ya hadhara, huo ni ubaguzi na upendeleo wenyewe.

"Jeshi la Polisi litimize wajibu wake kwa mujibu wa sheria bila upendeleo wowote na watende haki kwa vyama vyote, wakifanya hivyo hapatakuwa na malalamiko," alisisitiza Mrema.


**TSCHUDI TANZANIA LIMITED**
**Cheti cha Usajili Namba 155877022**
**Sheria ya Makampuni, 2002**
**(KIFUNGU 334 (1))**

**MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI**

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha **TSCHUDI TANZANIA LIMITED** (kampuni), yenye usajili namba 155877022, kilichofanyika tarehe 2 October 2024 azimio maalumu lilipitishwa:

1. Kufuatana na kifungu 333(1)(b) cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kuwa kampuni ifutwe kwa hiari; na
2. Wanahisa wamemteua NEEMA RICHARD wa Mikumi House, 368 Msasani Road, Oysterbay, S.L.P 9673, Dar es Salaam, Tanzania kuwa mfilisi wa kampuni.

Umma na wahusika wanafahamishwa kupeleka madai yao kwa usaili ndani ya siku thelathini (30). Maombi yote yatayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa.

NEEMA RICHARD
MFILISI WA TSCHUDI TANZANIA LIMITED



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
17/10/2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **18/10/2024** kampuni ya **AFRICA WAKAWAKA LOGISTICS CO. LTD** itasafirisha mzigo mkubwa kutoka Dar es Salaam kuelekea Tunduma kupitia Mikumi.
2. Gari hizo zenye namba za usajili:
   1. **T 469 EBS / T 360 EBR**
   2. **T 563 EHK / T 992 EBX**
   3. **T 285 EJG / T 764 EJE**

   VIPIMO
   **Urefu - 22M**
   **Upana - 4.95M,**
   **Kimo - 5.2M**
3. Gari litasafirisha mzigo kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## HABARI KITAIFA

# Mkulima kuwaburuza kortini vigogo kwa tuhuma kushusha bei ya pamba

**Na Remmy Moka,** MWANZA

MKULIMA wa pamba, Thomas Nkola, mkazi wa mkoani Simiyu, ameeleza nia ya kuwashtaki baadhi ya wabunge na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), akiwatuhumu kuingilia na kushusha bei ya pamba mkoani Simiyu na kuwasababishia hasara wakulima.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza juzi, mkulima huyo alisema pamba ni uti wa mgongo kwa wakazi na wakulima wa Simiyu, lakini wakulima hao wamekuwa hawanufaiki na kilimo hicho kutokana na watu wachache, wakiwamo wabunge, kutajinufaisha nacho.

Nkola alisema yupo katika hatua za mwisho za kufungua kesi dhidi ya baadhi ya wabunge wa majimbo ya mkoa huo na jimbo moja la mkoani Tabora.

Alisema lengo la kuwaburuza vigogo hao ni kutokana na madai kwamba wameshindwa kuwajibika kwa nafasi zao kuhakikisha kunakuwa na ununuzi mzuri wa pamba, huku baadhi yao wakidaiwa kulazimisha kuwa wanunuzi wa zao hilo.

"Kesi hiyo itahusisha pia viongozi waandamizi wa CCM na viongozi wa Bodi ya Pamba na wengine ambao wote hao wameingia katika bodi ya pamba kinyume cha utaratibu na kushusha bei yake kwa manufaa yao binafsi," alidai Nkola.

Alidai kuwa hivi sasa mfuko mmoja wa mbegu ya pamba unauzwa kwa Sh. 10,000 na viwatilifu kwa kila ekari moja vinagharimu Sh. 15,000, jambo linalosababisha wakulima kutofaidika na kilimo wakati wa mavuno.

Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Mkoa wa Simiyu, Robert Mafuru, alisema chama chao kinaungana na mkulima huyo kuhakikisha wakulima wa mkoa huo wanapata haki yao kupitia kilimo cha pamba.

Mafuru alisema falsafa ya chama hicho inahimiza maendeleo, hivyo hakuna budi kumuunga mkono mkulima huyo katika hatua zote za ufunguzi wa kesi na kuhakikisha wakulima wote wananufaika na pamba.

"Tupo tayari kumpatia wanasheria watakaosimamia kesi hiyo na kuhakikisha haki inapatikana kwa maslahi mapana ya wakulima wa zao la pamba mkoani Simiyu," alisema Mafuru.

# Wachoma nyumba madai kulipiza kisasi mauaji bodaboda mwenzao

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WATU wanaodaiwa kuwa madereva wa bodaboda wanadaiwa kuchoma nyumba ya Adili Mpambula wa mtaa wa London, Kata ya Lizaboni, Manispaa ya Songea kwa tuhuma za kumwua dereva mwenzao, Sharif Luambano, ambaye ni mkazi wa eneo hilo.

Chanzo cha mauaji hayo kinadaiwa kuwa ni deni la marejesho ya pikipiki kwa mkataba ambao ulikuwa umebaki miezi miwili kumalizika.

Mbali na kuchoma nyumba hiyo, wananchi hao pia waliweka magogo kuzuia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwenda kuzima moto katika nyumba hiyo iliyokuwa inateketea. Baadaye jeshi hilo lilipita na kufika kwenye nyumba hiyo lakini ilikuwa imeshateketea.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana, Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ruvuma, Merania Nyambwinyo, alisema kuwa akiwa ofisini Octoba 15, mwaka huu, majira ya saa 5:00 asubuhi, alipokea taarifa ya nyumba kuteketea kwa moto, hivyo kujiandaa kwenda kwenye tukio hilo.

Kamanda Nyambawinyo alisema walipofika jirani na eneo la tukio, ghafla waliona mbele yamewekwa magogo makubwa barabarani na walipósimama, walisikia sauti za watu wakisema gari la zimamoto lisifike kwenye eneo la tukio na hakuna mtu kuondoa magogo.

Hata hivyo, alisema baadaye walifanikiwa kuyaondoa magogo hayo kisha kupita na askari walipofika kwenye eneo la tukio, walikuta nyumba yote imeteketea kwa moto.

Alisema nyumba hiyo yenye vyumba vitatu, sebule na banda la vyumba vitatu nyuma na mali zote zilizokuwamo ndani, ziliteketea.

Chanzo cha tukio hilo alisema ni madai kwamba Mpambula alimuua jirani yake kwa kumjeruhi kichwani na kumsababishia kifo kisha alikimbia na kutokomea kusikojulikana.

Alisema wananchi walilizuia gari la zimamoto kwa madai kuwa wamechoma nyumba hiyo kwa sababu mmiliki ameuua mwenzao.

Kutokana na tukio hilo, kamanda huyo wa zimamoto aliwashauri wananchi kuacha kujichukulia sheria mkoni kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria. Alisema wananchi hao kama wasingeweka magogo hayo kulikuwa na uwezekano mkubwa wa kuokoa baadhi ya mali zilizokuwamo ndani ya nyumba hiyo.

Diwani wa Lizaboni, Odo Mbunda, alisema Luambano ambaye alikuwa Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tawi la Amani, aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani na jirani yake Mpambula ambaye alikuwa anadai fedha za marejesho ya pikipiki waliyowekeana mkataba baada ya muda wa mwaka mmoja alipaswa kuendelea kumiliki pikipiki hiyo ambayo ilibaki marejesho ya miezi miwili.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Fadhili Mdemu, alisema Luambanioo kabla ya kufikwa na umauti, Oktoba 14, mwaka huu, majira ya saa 2:00 usiku, alijeruhiwa vibaya kwa kupigwa na kitu kizito kichwani na Mpambula. Alisema baada ya kujeruhiwa, alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma mjini Songea ambako alifariki dunia akiwa anapatiwa matibabu.

Mdemu alisema mtuhumiwa alitoroka baada ya kutenda tukio hilo na kwamba juhudi za kumtafuta zinaendelea.

Alisema kutokana na kitendo hicho, kundi la madereva bodaboda walijichukulia sheria mkononi kwa kuvamia nyumba ya Mpambula na kuchoma moto nyumba hiyo na kuteketea.

Kamanda Mdemu alisema hakuna madhara yoyote kwa binadamu na kwamba upelelezi wa tukio hilo unaendelea ikiwa ni pamoja na kuwasaka watuhumiwa wote waliohusika kuichoma nyumba hiyo na kuzuia gari la zimamoto lililokuwa linakwenda kufanya uokoaji.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Beatrice Mwinuka (aliyevaa suti nyeusi), akitoa elimu ya umuhimu wa wananchi kujiandikisha katika Daftari la Mpigakura wilayani humo, wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala, aliyoifanya Kata ya Mpeta jana. **PICHA: HAMISI NASRI**

# TRA yataja sababu madeni makubwa wafanyabiashara

**Na Halfani Chusi**

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda, amesema moja ya sababu za baadhi ya wafanyabiashara kuwa na madeni makubwa ya kodi kipindi cha nyuma ni kutokana na kutofautiana kwa rekodi.

Amesema kutokana na changamoto hiyo, kuanzia Januari, mwakani, serikali itaanzisha mpango wa kuwekeza katika Mfumo wa Kodi za Ndani (IDRAS) ambao utasaidia kuondoa changamoto hiyo na zile za migogoro ya kikodi na kurahisisha ukusanyaji.

Mwenda aliyasema hayo jana katika kikao maalumu kilichoandaliwa na mamlaka hiyo kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kujadili namna bora ya kukusanya kodi na kuondoa vikwazo katika taasisi za kifedha.

Alisema lengo la kikao hicho ni kujadili namna ya kukuza biashara kwa taasisi za kifedha na kurahisisha upatikanaji wa kodi ambayo ndio msingi wa maendeleo ya nchi.

Mwenda alisema hatua ya mwisho kwa watakaokuwa wakaidi kulipa kodi watatumia mawakala wa benki japo zipo njia ambazo watazitumia awali kabla ya kufikia hatua hiyo.

"Kwanza hatuwezi kutumia wakala wa benki bila kumpeleka mlipakodi 'demand note' (taarifa kwa mhusika kumhitaji alipe) lakini pia hatuwezi kufanya hivyo bila kupeleka 'reminder note' (taarifa ya kumkumbusha).

Hapo lazima tuwaite tukae nao tuwasikilize na tuwape fursa ya kulipa kidogo kidogo. Lazima tuwaandikie barua ya nia ya kutumia benki kama mawakala lakini njia hiyo haiwezi kutumika mpaka mimi nijiridhishe," alifafanua.

Hata hivyo, alisisitiza hatamani kufikia katika hatua hiyo kwa kuwa njia hizo ni ndefu na kwamba atahakikisha wanatumia njia nyingine kufikia suluhu.

"Tutakaa nao tutajenga uhusiano ili tukubaliane namna bora ya wao kulipa madeni na kuwashauri waendelee kutumia huduma za kibenki kwa kuwa itawaweka katika nafasi ya kupata mikopo mikubwa kwa ajili ya kuendesha biashara zao.

Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, alisema majadiliano hayo ni ya kuangalia namna ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwezesha taasisi za kifedha kusaidia shughuli za kibiashara ili kuongeza ukusanyaji wa kodi.

Alisema benki ni miongoni mwa taasisi zinazolipa kodi kubwa na inatumika kama mawakala wa kukusanya kodi na kutunza fedha za walipakodi na kwamba kutokana na umuhimu huo kuna haja ya kuwa kitu kimoja ili kuboresha mazingira hayo.

Akizungumza kwa niaba ya benki zingine na taasisi za kifedha, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Theobald Sabi, alisema wamefurahi kukutanishwa na TRA na BoT kujadili masuala ya kodi na kufahamishwa hatua zilizochukuliwa.

Sabi alisema hatua hizo zitawapa wateja wao morali ya kuendelea kutumia kuweka fedha benki huku akisifu zitaleta matokeo chanya na kuwapa wateja imani kubwa ya kutumia mifumo rasmi katika biashara.

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email: customerrelations@guardian.co.tz**

MAKALA MAALUMU

# EJAT; Kipimo sahihi cha ubora wa uandishi wa habari Tanzania



Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe (kushoto), alikuwa miongoni mwa wageni wa EJAT 2023. Hapa akikabidhi tuzo kwa mmoja wa washindi.
**PICHA ZOTE: MCT**



Mwandishi Halfani Chusi wa Nipashe (kulia), akipokea Tuzo ya Mwandishi Bora wa Habari za Haki za Binadamu 2023 (magazeti) .

**Na Mwandishi Wetu**

EJAT ni kipimo sahihi cha ubora wa uandishi wa habari nchini," anasema Halfani Chusi, mmoja wa waandishi wa habari wa gazeti Nipashe mkoani Dar es Salaam.

Chusi ambaye ni Mshindi wa Tuzo ya Mwandishi Bora wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2023, anasema tuzo hizo zina tija kubwa katika kuimarisha ubora wa maudhui ya vyombo vya habari nchini na kuongeza uwajibikaji serikalini.

Mwandishi huyo anasema tuzo hizo zinazoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na washirika kwa miaka 15 mfululizo sasa, ni fursa kwa waandishi wa habari na vyombo vya habari nchini kupima viwango vya ubora wa maudhui yao, hata kurekebisha upungufu unaoibuliwa na jopo la majaji.

"Kwa miaka mitatu iliyopita niliandaa kazi zenye ubora na zilizochochea uwajibikaji serikalini na kuleta matokeo chanya katika jamii.

"Nimeona hakuna upendeleo wala uonevu kwa washiriki wa EJAT. Majaji wanaoteuliwa, wana uzoefu mkubwa katika tasnia ya habari. Mwandishi mwenye kazi bora ndiye anatangazwa mshindi.

"Sasa nina tuzo mbili za EJAT (Mwandishi Bora wa Habari za Haki za Binadamu 2021 na 2023). Tuzo hizi zimenipa nguvu ya kuandaa kazi bora zaidi. Zimetoa heshima kwa kazi nzuri ninazozifanya kuwezesha jamii kutatua matatizo yanayoikabili.

"Ni kengele kwangu kwamba kumbe ukiandaa kazi bora, zinalipa! Ninapaswa kuongeza ubora zaidi katika kazi zangu. Kazi zilizonipa ushindi, zilikuwa zimekamilika – nilifunua tatizo, nikalianika, wanaohusika wakazinduka, wakafuatilia, wakatekeleza na jamii ikapata furaha. Nilifuatilia utekelezaji wake katika kulitatua – mwanzo hadi mwisho," anasema.

Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe, anasema EJAT imeongeza hamasa kwa waandishi wa habari kujituma kazini na kuandaa kazi zenye ubora wa hali ya juu.

"Morali imeongezeka kwa waandishi wa habari, hasa kufanya habari za uchunguzi. Lile tatizo la habari zenye chanzo kimoja cha habari linatoweka, kwa sababu wanajua habari zinazotakiwa EJAT na kwingineko kwenye mashindano ya kitaaluma, ni zenye vyanzo vingi vya habari.

"Kwa hiyo, EJAT imeongeza hamasa kubwa kwa waandishi kuandaa kazi zenye ubora, ndio maana kila mwaka tumekuwa tukishuhudia ongezeko kubwa la kazi zinazoshindanishwa," Mhariri Mtendaji Beatrice anasema.

Ni hoja inayosadifu taarifa ya Mwenyekiti Kamati ya Maandalizi ya EJAT 2023, Ernest Sungura ya Septemba 28 mwaka huu wakati wa utoaji tuzo hizo jijini Dar es Salaam. Sungura alisema kuwa kazi zilizowasilishwa kwa ajili ya EJAT 2023 zilikuwa 1,135 kulinganisha na kazi 893 za EJAT 2022. EJAT 2020 ilikuwa na 396 na EJAT 2021 kazi zilikuwa 608.

Sungura ambaye ni Katibu Mtendaji wa MCT, alisema kuwa kwa EJAT 2023, waandishi wa habari wa mkoa wa Dar es Salaam waliongoza kwa kuwasilisha kazi 290, wakifuatwa na mkoa wa Arusha uliokuwa na kazi 81, Mwanza (74), Iringa (72) wakati mkoa wa Mtwara ulishika nafasi ya tano kwa kuwa na kazi 49.

Kwa upande wa Zanzibar, kazi zilizopokewa ni kutoka Kaskazini Pemba (36), Pemba Kusini (43) na Mjini Magharibi (29).

Sungura alisema Jopo la Majaji wa EJAT 2023 lilichaguliwa na wakuu wa taasisi za kihabari zinazounda Kamati ya Maandalizi ya tuzo hizo kwa kuzingatia uadilifu, ujuzi na uzoefu katika uandishi wa habari, uwezo wa kuchambua na kutoa tathmini sahihi, uelewa wa mabadiliko ya kidigitali na uzoefu wa kimataifa au wa kijamii.

Jopo hilo liliongozwa na Halima Shariff, katibu wake Dk. Egbert Mkoko na majaji wengine wakiwa ni Mkumbwa Ally, Eshe Muhiddin, Jeniffer Sumi, Halima Msellemu na Absalom Kibanda.

Sungura alisema kuwa katika mchakato wa kuwapata majaji hao, kamati ilizingatia pia uwiano wa kizazi kipya na cha zamani, waliopo kazini na waliostaafu, wabobezi wa maudhui mahsusi, usawa wa kijinsia, uwakilishi wa Zanzibar na Tanzania Bara na uwakilishi wa aina ya vyombo vya habari (magazeti, redio, luninga na mitandao).

Taasisi zinaounda Kamati ya Maandalizi ni Wakfu wa Vyombo vya Habari (TMF), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Jukwaa la Wahariri (TEF), HakiElimu, Umoja wa Waandishi wa Habari za Mazingira (JET), Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Umoja wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT), Sikika, Misa - Tan na Twaweza.



Msanifu Mkuu wa Nipashe, Sanula Athanas (kulia), akipokea Tuzo ya Mwandishi Bora wa Habari za Elimu Mwaka 2023 (magazeti). Athanas pia aliibuka mshindi katika kipengele cha Kundi la Wazi (magezeti).

Kwa mujibu wa Sungura, wateule 72 wa EJAT 2023 walipatikana kwa kukidhi vigezo vya ubora ambavyo ni pamoja na ukweli, usahihi, uanuai, haki, kina, utafiti, ubunifu, uvumbuzi, upekee, uchambuzi, uwajibikaji, ufichuaji maovu, uadilifu, uwasilishaji unaoeleweka na uchunguzi.

"Ifahamike pia kwamba vigezo maalumu vilitumika kuzingatia aina tofauti ya vyombo vya habari kama vile redio, televisheni, magazeti na habari za mitandaoni," Sungura alisema.

EJAT 2023 imekuwa na mambo kadhaa ya kipekee ambayo hayakushuhudiwa katika miaka 14 iliyotangulia ya tuzo hizo: Kwa mara ya kwanza, mshindi wa Jumla ametoka Zanzibar, pia kwa mara ya kwanza ametoka kwenye vyombo vya habari vya mtandaoni.

Jambo la pili la kipekee ni uzinduzi wa Jarida la Tuzo (moja la Kiswahili na lingine la kwa lugha ya Kiingereza), yakijikita kuhamasisha umahiri katika sekta mbalimbali Tanzania na nje ya Tanzania. Sungara alisema kuwa kwa kuanzia, majarida hayo yatabeba maudhui ya EJAT, yakiangazia simulizi ya maisha ya wateule wote na wafadhili wa tuzo.

Vilevile, hafla ya utoaji tuzo hizo mwaka huu ilikuwa ya kipekee; ilirushwa moja kwa moja kupitia runinga za Channel Ten, TBC1 na UTV.

Ilikuwa EJAT ya kwanza kwa Katibu Mtendaji mpya Sungura. EJAT 14 zilizotangulia, zilifanyika chini ya Katibu Mtendaji Kajubi Mukajanga. Katibu Mtendaji wa MCT ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT.

Makundi yaliyoshindaniwa kwa EJAT 2023 ni pamoja na Tuzo ya Uandishi wa Habari za Biashara, Uchumi na Fedha; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Utamaduni na Michezo;

Tuzo ya Uandishi wa Habari za Kilimo na Biashara ya Kilimo; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Elimu; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Utalii na Uhifadhi; na Tuzo ya Uandishi wa Habari za Uchunguzi.

Makundi mengine ni Tuzo za Uandishi wa Habari za Data; Tuzo za Uandishi wa Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Jinsia na Watoto; Tuzo za Uandishi wa Habari za Walemavu; Tuzo za Uandishi wa Habari za Afya; Tuzo za Uandishi wa Habari za Ushirika; na Tuzo za Uandishi wa Habari za Kodi, Tozo na Mapato.

Mengine ni Habari za Uandishi wa Habari za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Utunzaji wa Mazingira na Vyanzo vya Maji; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Afya ya Uzazi; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto; Tuzo ya Uandishi wa Habari za Mafuta, Gesi na Uchimbaji Madini na Kundi la Wazi.

HABARI KITAIFA

# Mpango waja kuiweka Sinza katika sura mpya

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaandaa mpango wa uendelezaji upya eneo la Sinza, Dar es Salaam ujulikanao kama Sinza Redevelopment Plan 2024 - 2044.

Hayo yalibainishwa jana mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii wakati wa uwasilishaji taarifa ya mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi (KKK).

Akiwasilisha taarifa ya mpango huo, Mratibu wa Mradi wa KKK, Godfrey Machabe, alisema wizara inaandaa mpango wa uendelezaji upya wa maeneo kongwe katika mkoa wa Dar es Salaam.

"Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa Ubungo pamoja na wadau wengine, wizara imeandaa Mpango wa Uendelezaji Upya Eneo la Sinza," alisema.

Machabe alibainisha kuwa mpango wa uendelezaji upya katika eneo hilo ni mkakati wa kina kwa ajili ya kufufua maeneo ambayo yamezorota na kupoteza thamani pamoja na uhalisia.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, mpango huo unatekelezwa kutokana na sababu mbalimbali kama vile ukuaji wa kasi na majengo marefu, ongezeko kubwa la watu na shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii pamoja na ongezeko la uhitaji wa huduma za kijamii na miundombinu.

Mpango huo umepanga kujumuisha mabadiliko ya matumizi ya ardhi, kujenga na kuboresha miundombinu na kuboresha huduma za jamii na miundombinu ya huduma za jamii kama vile usafiri, maji safi, majitaka, maji ya mvua, umeme, taka ngumu, mifumo ya gesi, nishati ya umeme na mawasiliano.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya mwenyekiti Timotheo MNzava, imeridhishwa na utekelezaji wa mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi unaotekelezwa na wizara kwenye maeneo mbalimbali nchini.

"Tumeridhishwa na utekelezaji mradi wa KKK ukiwamo huu mpango wa kuendeleza maeneo kongwe likiwamo eneo la Sinza," alisema Mnzava.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, alisema wizara inafuatilia maeneo ya miji mikongwe kwa lengo la kuona namna ya kuyaboresha ili kuendana na kasi ya ukuaji wa maendeleo.

Kuhusu mradi wa KKK katika mwaka 2023/24, Pinda alisema wizara ilihuisha akaunti ya Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi (PDRF) kwa ajili ya utekelezaji miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi. Alisema mfuko huo utakuwa ukitoa fedha kwa halmashauri kutekeleza miradi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi.

Kwa mujibu wa Pinda, mfuko huo umeandaliwa mwongozo wa uratibu na utekelezaji kwa ajili ya kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipokea na kujadili taarifa za Wizara ya Ardhi zinazohusu Utekelezaji Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK), hatua iliyofikiwa katika uandaaji wa Sera ya Ardhi pamoja na taarifa ya hatua iliyofikiwa kwenye Uanzishwaji wa Mamlaka ya Sekta ya Milki.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati), akizungumza jambo na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Maendeleo ya Ushirika na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), Mrajisi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Dk. Benson Ndiege (kulia), Mwenyekiti wa Bodi ya CBT, Prof. Gervas Machimu (wa pili kulia), na Mkurugenzi Mtendaji wa CBT, Godfrey Ng'urah, wakati alipowasili katika mkutano mkuu wa kwanza wa Benki ya Ushirika Tanzania (CBT) uliofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nsekela, TCDC wamkosha Bashe uanzishwaji wa Benki ya Ushirika

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

BENKI mpya ya Ushirika ya Tanzania (CBT) imefanya Mkutano Mkuu wake wa Kwanza wa Mwaka (AGM), ikiwa ni hatua muhimu katika maendeleo ya sekta ya ushirika nchini.

Ni hatua inayoshuhudiwa ikiwa ni miezi michache baada ya muunganiko wa Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (KCBL) na Benki ya Jamii ya Tandahimba (TACOBA), ambao ulikamilika tarehe 26, Mei 2024.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe amesema kuanzishwa kwa benki hiyo ni ushahidi wa uongozi wa kimaono wa Abdulmajid Nsekela, Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), ambaye moja ya vipaumbele vyake baada ya kuteuliwa na Rais Samia ni kuharakisha mchakato wa uanzishwaji benki ya kitaifa ya ushirika.

Benki hiyo ambayo sasa imesajiliwa rasmi na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), inafanya kazi kama taasisi ya kibiashara inayohudumia sekta ya ushirika na soko kwa ujumla.

Tofauti na taasisi nyingine za kifedha zinazomilikiwa na serikali, CBT inamilikiwa kimsingi na vyama vya ushirika na wanachama wake (asilimia 51), huku serikali ikishikilia hisa ya asilimia 10, na asilimia 39 iliyobaki inamilikiwa na watu binafsi na kampuni.

Hisa za ushirika zimehifadhiwa mahsusi kwa wanachama wa ushirika pekee na zinaweza kuuzwa na kununuliwa miongoni mwao. CBT imejipanga kimkakati kuhudumia mnyororo mzima wa thamani wa biashara za ushirika, ikitoa huduma za kifedha zenye ushindani kwa lengo la kuwawezesha ushirika na kukuza ujumuishi wa kifedha.

Wakati wa mkutano huo, Waziri Bashe alipongeza mafanikio ya kuanzishwa kwa CBT, akihusisha mafanikio yake na umahiri wa uongozi wa Nsekela.

"Kuzinduliwa kwa CBT ni mabadiliko makubwa kwa harakati za ushirika hapa Tanzania," alibainisha waziri huyo huku akimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuunga mkono hatua ya kuanzisha benki hiyo kwa kutoa Sh. bilioni tano na kuruhusu serikali kumiliki hisa ndani ya CBT.

Waziri Bashe alitangaza kuwa Rais Samia atazindua rasmi benki hiyo katika hafla kubwa hivi karibuni. Alihimiza vyama vyote vya ushirika vilivyo chini ya Wizara ya Kilimo kuchangamkia fursa ya benki hiyo kwa kufungua akaunti na kufanya biashara kupitia CBT.

Ili kuimarisha hilo, alimwagiza Msajili wa Vyama vya Ushirika kuhakikisha miamala yote ya kilimo, kama vile mauzo ya korosho katika mikoa ya kusini, inasimamiwa kupitia CBT.

Wakati CBT ikiangazia kupanua wigo wake wa huduma, tayari inafanya kazi kupitia matawi yake ya Moshi na Tandahimba, huku tawi jipya likitarajiwa kufunguliwa Dodoma ifikapo Novemba na lingine Tabora kabla ya Desemba mwaka huu.

Benki hiyo pia ina ushirikiano wa kimkakati na Benki ya CRDB, ambayo pia ni mwekezaji ndani ya CBT kwa asilimia 20, ikiruhusu wateja wa CBT kutumia mitandao ya ATM na mawakala wa CRDB Wakala nchi nzima wakati huu wa mpito.

Katika hotuba yake, Mwenyekiti wa TCDC, Nsekela, alisisitiza dhamira yake ya kubadilisha mfumo wa ushirika wa Tanzania kuwa wenye ushindani, uaminifu na manufaa kwa wanachama wake.

Alieleza furaha yake ya kuona mwendelezo wa kukamilisha vipaumbele saba ambavyo bodi yake iliviainisha vinavyolenga kuboresha na kuimarisha sekta ya ushirika, huku kipaumbele kikubwa kikiwa ni mifumo ya kidijitali na uanzishwaji CBT.

## Adha ya usafiri wa boti yaikumba Mafia

**Na Julieth Mkireri**

WAKAZI wa Wilaya ya Mafia Mkoa wa Pwani wamelalamikia kukosekana kwa usafiri wa boti kwa kipindi cha wiki moja sasa hali inayowalazimu kutumia majahazi na boti za wavuvi kutokana na kushindwa kumudu gharama za usafiri wa ndege.

Wakizungumza kwa njia ya simu na Nipashe juzi, baadhi ya wakazi hao walisema tatizo hilo la usafiri linawasababishia kutumia siku mbili hadi tatu kufika Nyamisati Wilaya ya Kibiti, tofauti na meli ambayo inachukua saa nne hadi tano.

Mmoja wa wakazi hao, Karim Mohamed, alisema serikali inatakiwa kuthamini kisiwa cha Mafia kama ilivyo kwa visiwa vingine kwa kuwa kuna watu wanahitaji huduma muhimu za kijamii na usafiri ukiwa muhimu kwa ajili ya kufuata mahitaji muhimu Dar es Salaam kwa muda wote.

Alisema kipato cha wakazi wa Mafia ni cha hali ya chini na si wote wanaweza kumudu gharama za ndege jambo ambalo linawalazimu kutumia majahazi na boti za wavuvi kusafiri wakati huu wakisubiri meli kutengamaa.

Naye Khatibu Hamis alisema ndani ya wiki moja ambayo hakuna meli, usafiri unaotumika si salama kwa abiria wanaoutumia kwa kuwa unakaa muda mrefu kwenye maji lakini pia mzunguko majini ni mkubwa ukilinganisha na meli.

Hussein Mbaruk alisema kitendo cha kukosekana usafiri wa uhakika kwa wakazi wa Mafia kwa kipindi hiki unaweza kuathiri baadhi ya wananchi kushindwa kujiandikisha katika Daftari la Wakazi kwa kuwa wako wanaopiga kura katika wilaya zingine za Pwani na Dar es Salaam na hadi sasa wako Mafia na wengine wako Mafia ambao wameshindwa kurejea kwao.

Mbaruk aliiomba serikali kutafuta usafiri wa uhakika wa meli ambayo ni imara kwa ajili ya kusafirisha wananchi wa kisiwa hicho ili kuondoa tatizo hilo ambalo limekuwa likijitokeza mara kwa mara huku wengi wao wakishindwa kumudu gharama za ndege.

"Yaani hii meli ikipona leo baada ya muda utasikia kuna hitilafu wananchi wanarudi kuhangaika na usafiri tena. Tunaomba serikali iangalie hili kwa sasa hata mgonjwa akipewa rufani kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kama uwezo wake ni mdogo hawezi kwenda tena," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), Alfred Mgweno, aliimbia Nipashe kwamba kivuko kilichokuwapo kilipata hitilafu kwenye injini baada ya moja kufa na ikabaki moja inayofanya kazi, hivyo kusimama kutoa huduma.

Mgweno aliwaomba wananchi kuwa wavumilivu wakati ukarabati wa kivuko hicho ukiendelea kufanyika huku akiwasihi kuepuka kutumia usafiri ambao si salama kwao.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tatizo usafiri wa boti Mafia lichukuliwe kwa uzito mkubwa

**KUMEKUWAPO** na taarifa kwamba wakazi wa kisiwa cha Mafia katika mkoa wa Pwani, wanalalamikia kukosekana kwa usafiri wa uhakika wa boti kwa takriban wiki mbili sasa.

Sababu kubwa ya kukosekana kwa usafiri huo unaotegemewa na wengi, kwa mujibu wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), kivuko kilichokuwapo kupata hitilafu kwenye injini baada ya moja kufa na ikabaki moja inayofanya kazi, hivyo kusimama kutoa huduma. Kutokana na tatizo hilo, TEMESA imewaomba wananchi hao kuwa wavumilivu na kuacha kutumia usafiri usio salama kama wa kutumia mitumbwi.

Kutokana na kukosekana kwa usafiri huo, wananchi wa kisiwa hicho wamejikuta wakilazimika kutumia mitumbwi kwenda katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kutafuta mahitaji. Kwa mujibu wa wananchi hao, kwa kukosekana kwa boti inayotoka na kuingia kisiwani humo, wanatumia majahazi na boti za wavuvi kutokana na kushindwa kumudu gharama za usafiri wa ndege.

Aidha, sehemu inayofungua milango ya mawasiliano kati ya Mafia na maeneo mengine ni Nyamisati wilayani ambako baada ya kufika wanaweza kusafiri kwa aina nyingine ya usafiri na hatimaye kupata mahitaji yao muhimu. Kutokana na kutokuwapo kwa boti hiyo, walisema wanasafiri hata kwa siku mbili hadi tatu kufika Nyamisati tofauti na saa nne hadi tano wanazotumia kukiwapo boti.

Tatizo hilo pia limesababisha hata wagonjwa wanaohitaji rufani kwenda Dar es Salaam au hospitali zingine kubwa kwa matibabu kuwa katika wakati mgumu hata hatari ya kupoteza maisha. Licha ya wagonjwa, pia wananchi wanashindwa kupata mahitaji muhimu ambayo mengi yanapatikana Dar es Salaam.

Kwa jumla, wananchi wengi wa kisiwa cha Mafia ni wa kipato cha chini, hivyo unapokosekana usafiri wa meli au boti ya uhakika, wanakuwa wamefungwa. Hali hiyo ni kwa sababu wanaoweza kutumia usafiri wa anga, kwa maana ya ndege ni wachache. Kwa mantiki hiyo, kutokuwapo kwa usafiri wa majini kunawafanya wakose mahitaji muhimu, kama vile vyakula na vinywaji, ambayo mengi yanatoka maeneo ya nchi kavu kama Kibiti, Dar es Salaam na Mkuranga.

TEMESA imetoa ufafanuzi kwamba kukosekana kwa usafiri huo kunatokana na kufa kwa injini moja kati ya mbili za boti hiyo, hivyo kulazimika kuipelekwa kwenye matengenezo. Sababu hiyo ni nzuri kwa usalama wa chombo hicho lakini haitoshi bali taasisi hiyo ilipaswa kuchukua hatua ili kuwa na usafiri wa muda wakati ule wa uhakika unapofanyiwa matengenezo.

Kwa kuzingatia mazingira na umuhimu wa mahitaji ya wananchi wa kisiwa cha Mafia, serikali kupitia TEMESA ilipaswa kukodi boti ili kuwawezesha kupata usafiri badala ya kuwaacha wakiteseka kama ilivyo kwa zaidi ya wiki sasa.

Hivi karibuni kulikuwa na shida ya usafiri wa boti kati ya Feri na Kigamboni mkoani Dar es Salaam lakini kutokana na mahitaji makubwa ya usafiri huo, serikali ilichukua hatua kwa kutumia boti za biashara kukwamua tatizo. Inakuwaje jambo kama hilo kushindikana kwa kisiwa cha Mafia ambacho usafiri mkubwa unaotegemewa na wananchi wengi ni wa boti?

Kutokana na uhalisia wa mazingira katika kisiwa cha Mafia, serikali kupitia TEMESA, inapaswa kuchukua hatua za haraka kuhakikisha usafiri wa uhakika unapatikana na kuwaondolewa adha wananyoipata kwa sasa. Majibu ya TEMESA ni mepesi kwa maswali magumu hasa kutokana na mazingira wanayokabiliwa nayo wananchi katika kisiwa cha Mafia.

Suala hili halipaswi kuchukuliwa kwa uzito mwepesi kama majibu yaliyotolewa bali kuchukua hatua stahiki kwa uzito mkubwa. Wananchi wa Mafia wanachohitaji si kuwataka wawe na uvumilivu bali majibu kwamba tatizo lao litashughulikiwa na kumalizika kwa namna gani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

## Inapotangazwa operesheni mambo haya ya saratani, tuungane kusaka

**UGONJWA** wa saratani upo katika maeneo mbalimbali ya mwili wa mwanadamu. Ni maradhi yanayowapata watu wa aina yoyote na hauchagui rika.

Ni ugonjwa ambao unatokana na visababisha mbalimbali. Baadhi ya jamii huhisi kuna saratani ya matiti na shingo ya uzazi.

Ugonjwa wa saratani upo katika makundi mbalimbali, huku jamii inaweza kwa jumla kupata ugonjwa huo. Kuna saratani ya koo, saratani ya shingo ya kizazi, damu na saratani ya matiti.

Katika kukabiliana na ugonjwa huo, serikali imekuwa ikitoa elimu kwa jamii ili isipate magonjwa hayo ambayo imeonekana kila mwaka yanaongezeka.

Hivi karibuni serikali kupitia Wizara ya Afya, imeendelea kushirikiana na wadau kutokomeza ugonjwa huo nchini na serikali inatoa elimu kwa jamii, pamoja na kuhimiza upatikanaji wa chanjo, mathalan dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana.

Kwa kuwa ugonjwa huo umekuwa ukiongezeka kila mwaka, serikali imejipanga kupambana nayo kwa kuboresha mahitaji ya huduma hiyo katika hospitali na vituo vya afya.

Waziri wa Afya, Jenister Mhagama, anasema hayo katika ufunguzi wa kituo cha saratani kilichoko katika Hospitali ya Shufaa iliyoko jijini Dar es Salaam, akinena:

"Ufunguzi wa kituo hiki utaongeza upatikanaji wa huduma za uchunguzi na matibabu ya saratani hapa nchini kwa kuwa tatizo la ugonjwa huo limekuwa likiongezeka hapa nchini," anasema.

Anaongeza kuwa takwimu za saratani hapa nchini kwa mwaka 2022, zimeonyesha wagonjwa wapya wako 48,000 na kati yao waliogundulika asilimia 24.4 ni saratani ya mlango wa kizazi.

Anaongeza kuwa saratani ya tezi dume waligundulika asilimia 10.7, saratani ya matiti asilimia 10 na saratani ya koo asilimia 7.9 na saratani ya utumbo asilimia 4.9.

"Saratani hizi zinachukuwa karibu nusu ya asilimia 42.2 ya wagonjwa wote wa saratani hapa nchini," anasema.

Anaongeza kuwa saratani mbili zinaziathiri zaidi wanawake ni saratani ya mlango wa uzazi na saratani ya matiti ndio zinachukuwa theluthi moja ya wagonjwa wote wa saratani hapa nchini.

Anasema, kufuatia kuongezeka kwa saratani nchini, serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo utoaji wa elimu ya afya pamoja na kuimarisha huduma za uchunguzi wa saratani ya mlango wa uzazi katika hospitali ikiwamo na vituo vya afya hapa nchini.

Anaongeza kuwa wajibu wao kama serikali ni uthibiti wa ubora na sio udhibiti wa sekta binafsi kukua, wataendelea kushirikiana na sekta binafsi kwa pamoja ili waweze kutoa huduma iliyo bora na salama kwa wananchi.

Waziri anasema, ili kuongeza ufanisi katika huduma za uchunguzi.

Pia serikali imeimarisha upatikanaji huduma za uchunguzi wa maabara na uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye huduma za radiolojia kwa kuimarisha upatikanaji vipimo vya kisasa ikiwamo vifaa; CT Scan 85 katika mikoa yote 26 nchini.

Sasa cha muhimu kwetu site ni pale juhudi na hatua kama hizo zinachukuliwa na serikali kutetea nafasi ya afya zetu, sote tujitahidi katika nafasi yetu kuunga mkono katika namna mbalimbali, ikiwamo kujitokeza katikia chanjo na tiba.

Pia, kila mmoja mwenyewe katika nafasi yake inapaswa kujitahidi kutambua na kuna fursa ya kijamii, huku ikitangaza katika namna mbalimbali kufuata hatua ya mafanikio katika eneo hilo.

TANGAZO

tigo pesa

# Ni Zaidi ya Pesa

## Ada za wateja. Piga *150*01#

| Kiwango (Tsh) | | Kutuma pesa kwenda Tigo Pesa | Kutuma pesa kwenda Mitandao washirika | Kutoa pesa kwa Wakala/ATM | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzia | Mwisho | Ada ya Tigo Pesa | Ada ya Tigo Pesa | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato |
| 100 | 999 | 15 | 15 | - | 10 | 10 |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 45 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 30 | 45 | 400 | 10 | 410 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 90 | 600 | 14 | 614 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 90 | 650 | 27 | 677 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 180 | 950 | 54 | 1,004 |
| 7,000 | 9,999 | 150 | 180 | 1,000 | 56 | 1,056 |
| 10,000 | 14,999 | 360 | 495 | 1,450 | 102 | 1,552 |
| 15,000 | 19,999 | 360 | 495 | 1,450 | 195 | 1,645 |
| 20,000 | 29,999 | 380 | 540 | 1,850 | 306 | 2,156 |
| 30,000 | 39,999 | 400 | 612 | 1,850 | 351 | 2,201 |
| 40,000 | 49,999 | 410 | 675 | 2,350 | 419 | 2,769 |
| 50,000 | 99,999 | 720 | 1,125 | 2,700 | 573 | 3,273 |
| 100,000 | 199,999 | 1,000 | 1,440 | 3,650 | 707 | 4,357 |
| 200,000 | 299,999 | 1,200 | 1,710 | 5,300 | 821 | 6,121 |
| 300,000 | 399,999 | 1,500 | 2,070 | 6,500 | 838 | 7,338 |
| 400,000 | 499,999 | 1,500 | 2,250 | 7,000 | 982 | 7,982 |
| 500,000 | 599,999 | 2,200 | 2,880 | 7,500 | 1,245 | 8,745 |
| 600,000 | 699,999 | 3,300 | 3,870 | 8,000 | 1,532 | 9,532 |
| 700,000 | 799,999 | 3,300 | 3,870 | 8,000 | 1,700 | 9,700 |
| 800,000 | 899,999 | 3,500 | 3,870 | 8,000 | 1,750 | 9,750 |
| 900,000 | 1,000,000 | 3,500 | 5,400 | 8,000 | 1,776 | 9,776 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 5,000 | 5,400 | 8,000 | 1,875 | 9,875 |
| 3,000,001 | 10,000,000 | 5,000 | 5,400 | 10,000 | 2,000 | 12,000 |

| Tukio | Kuanzia | Mwisho | Ada |
|---|---|---|---|
| Kuweka pesa | 1,000 | 5,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwenda nchi za nje | 100 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |
| Malipo kwa Tigo Pesa | 500 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |

| Tukio | Ada |
|---|---|
| Kubadilisha namba ya siri | BURE |
| Kuangalia salio | BURE |
| Taarifa ndogo | 50 |
| Kurudisha muamala uliokosea (Jihudumie) | 50 |
| **Kupata taarifa ya mwezi** | **Ada** |
| Taarifa ya Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |
| Taarifa ya Miezi 3 | 1,000 |
| Taarifa ya Mwaka 1 | 2,000 |

Kwa vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-standard-terms-and-conditions. **Ada zote zimejumuisha kodi zote zinazohusika**
Kwa Ada za huduma nyingine tembelea **tovuti; https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-tariffs**

**Furahia Malipo kwa Tigo Pesa:**

LIPA KWA SIMU

**KUMBUKA:**
1. Unaweza kuweka au kupokea hadi TSh 5,000,000 kwa siku na unaweza kutoa au kutuma hadi TSh 5,000,000 kwa siku, pia unaweza kuhifadhi hadi TSh 10,000,000 kwa wakati mmoja kwenye akaunti yako ya Tigo Pesa, kama usajili wako umekamilika.
2. Onesha kitambulisho chako kabla ya kuweka au kutoa pesa kwa Wakala.
3. Hakikisha taarifa zako za usajili ni sahihi kwa kupiga *106# kisha 2 au piga huduma kwa wateja kwa maelezo zaidi.
4. Hesabu pesa zako na hakikisha salio lako la Tigo Pesa linaendana na muamala uliofanya kabla ya kuondoka kwa Wakala.
5. Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
6. Hakikisha unahifadhi namba yako ya siri (PIN), simu yako na laini yako kwa usalama. Usimpe (PIN, Simu, laini yako) wala kumtajia mtu yoyote namba yako ya siri, iwe Wakala wa Tigo Pesa, mfanyakazi wa Tigo au mhudumu wa Tigo Huduma kwa wateja. Pia kumbuka kubadili namba yako ya siri mara kwa mara.
7. Tigo itakupigia kwa 100 Tu.
8. Kutoa taarifa yoyote dhidi ya udanganyifu Piga simu namba 100 au tuma ujumbe kwenda namba 15040 au barua pepe kwenda customercare@tigo.co.tz
9. Unaweza kupokea pesa kutoka nchi zaidi ya 200 duniani, na unaweza kutuma pesa kwenda nchi zote za Mashariki na Kusini mwa Afrika .
10. Kupata vigezo na masharti ya kutumia Tigo Pesa, tembelea duka la Tigo lililopo karibu nawe au www.tigo.co.tz

Unaweza kurudisha **muamala uliokosea**, **kupata token ya luku, ku-unbar akaunti yako ya Tigo Pesa** na **kuriseti PIN**

Piga ***150*01#**
chagua **6 (Jihudumie)**
kisha chagua huduma unayotaka

tigo pesa

App yenye urahisi wa kushangaza!



**Fanya malipo ya Serikali**

TRA RITA DAWASA TANESCO LUKU

Pakua kwenye

Google Play | App Store

tigo pesa

www.tigo.co.tz

Kuwasaliana na huduma kwa wateja,
Piga **100** bure au tembelea duka lolote la Tigo!
Ada hizi ni kuanzia 01 Julai 2023

tigo

# MATANGAZO

DTB DIAMOND TRUST BANK

## Diamond Trust Bank yaandaa mchezo wa Gofu jijini Arusha

Diamond Trust Bank iliandaa mchuano wa mchezo wa gofu jijini Arusha mwisho wa juma uliowakutanisha wachezaji zaidi ya 70 wa mchezo huo – ikijumuisha wachezaji wanawake na wanaume. Tukio hili ni sehemu endelevu ya kujenga mahusiano na wateja pamoja na jamii kwa ujumla kwa kushiriki kwenye michezo na kubadilishana uzoefu katika maswahili ya kujenga uchumi.

Mashindano hayo yaliyofanyika katika Klabu maarufu ya Gofu ya Arusha Gymkhana, yalionyesha dhamira ya benki hiyo katika kukuza uhusiano mzuri na wateja wake na jamii kwa ujumla. Washiriki walifurahia siku hii kwa kuonyesha ujuzi wao katika mchezo huu wa gofu.

"Inafurahisha kuona wateja wetu waliopo Arusha na Kilimanjaro wanakusanyika katika mashindano kama haya na kushindana kwa lengo la kukuza mchezo huu wa gofu. Matukio kama haya ni muhimu katika kujenga uhusiano mzuri na wa kudumu kwa wateja wetu na jamii inayotuzunguka. tumefurahishwa na mafanikio ya mashindano hay ana tumenuia kuandaa mashindano haya na tumenuia kuandaa mashindano haya kila mwaka ili kuvutia wachezaji kutoka mikoa mingine pia" Alisema Bw. Ravneet Chowdhury, Afisa Mtendaji Mkuu wa Diamond Trust Bank.



*Afisa Mtendaji Mkuu wa Diamond Trust Bank Bw. Ravneet Chowdhury akizungumza na wachezaji wa gofu katika viwanja vya Arusha Gymkhana baada ya mchuano huo*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa Diamond Trust Bank Bw. Ravneet Chowdhury akikabidhi zawadi kwa mshindi kwa upande wa wanawake Bi. Adrie Brown*



*Afisa Mtendaji Mkuu wa DTB Bw. Ravneet Chowdhury akikabidhi kombe kwa mshindi wa pili Bw. George Ogutu*



*Mmoja wa wachezaji Bw. Hiten Nathwani akipiga mpira kwa umakini wakati wa mchezo huo ulioandaliwa na Diamond Trust Bank*

dtbtanzania

**Bank with us. Bank on us.**

---

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: PIPELINE ENGINEER**

**Reports to:** N+1: Inspection LeaderN+ 2: Maintenance and Inspection Head

**Job Type:** Full Time + 5d/w - with regular duty week and regular EACOP site visit

**Location:** MST - Tanga

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

Pipeline engineer will be part of EACOP inspection entity. He/she will manage pipeline inspection activity directly for PS4/PS5 and MST perimeters, for PS1 perimeter, he will provide support to the pipeline and inspection engineer. He/she will follow guidance and inspection philosophy from Inspection Leader. He/she will be in charge to define the pipeline corrosion guidance documents.
Pipeline engineer will be the main interface and focal point for pipeline integrity management and corrosion and chemical treatment follow up in Tanzanian perimeters. Corrosion coupons and intelligent pigging operation will be closely prepared and assisted by pipeline and inspection engineer. He/she will ensure inspection scope and campaign are completed.

**EACOP PS4,5 and MST perimeters main equipment under pipeline engineer responsibility are:**

- Pipeline
- Corrosion coupons
- EPRS (pipeline repair)

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

- Implements the Inspection Plans (written scheme of inspection) for the following equipment: PSD, pipelines, and pipeline related structure as HDD.
- Ensures that equipment registers, Inspection Plans scheduling, Inspection Reporting, Remedial actions are managed with the dedicated CMIMS (Computerized Maintenance & Inspection Management System) and RBI-P.
- Ensures that Inspections and Non-Destructive Testing are executed in compliance with the relevant Safety Rules, Inspection Plans, Technical Procedures and Standards.
- Ensures coordination of inspection activities on Site and supervision of inspection Contractors.
- Assists the Third-party representatives responsible for statutory inspections (Third Party certification, Authorities).
- Prepares / Reviews the Inspection Reports, including analysis of inspection findings, fit for service assessment, recommendation, or remedial actions.
- Prepares/reviews pipeline inspection and corrosion guidance document and procedure.
- Prepares/reviews SMC as intelligent pigging and corrosion coupons analysis and operations.
- Proposes / reviews the recommendations for corrective actions (material selection, design of equipment, coating, cathodic protection, operating conditions, corrosion inhibition…).
- Make sure that recommendations for remedial actions are issued in the CMIMS system and ensure their follow up.
- Ensures that repair / modifications / procurement of equipment comply with the relevant regulation, company rules, technical codes, and norms.
- Reviews management of change request when required.
- Participates in technical audits of contracted companies regarding Non-Destructive Testing, Welding, Piping / Pressure Vessel fabrication, Coating.
- Updates data required for Risk base inspection tools.
- Be the focal point for pipeline inspection and corrosion exchange for Tanzania pipeline section.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- Bachelor level or similar.
- Mechanics or Materials Engineer (or equivalent) with emphasis on mechanics, materials, metallurgy, and corrosion.
- Knowledge of Oil & Gas process equipment, technology, and pipeline.
- Good knowledge of international Codes, Standards and Regulation related to the inspection discipline (ASME, API, NACE…)
- Good knowledge of materials, metallurgy, welding, corrosion, failure modes, Non-Destructive Testing, and inspection techniques.
- Knowledge of RBI methodology (Risk Based Inspection)
- Good knowledge of CMIMS (Computerized Maintenance & Inspection Management System)
- Good knowledge in Fitness for Service assessment methods (API RP 579, ASME, DNV…)
- Proficiency in oral and written English.
- ERB Registration as a Professional Engineer.

**Experience Required:**

- Experience in NDT inspection technics minimum 2 years.
- Experience in corrosion analysis.
- Experience in pipeline inspection.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**



# Maji kwanza, wanakijiji wawapasha wagombea

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKAZI wa vitongoji vya Kijiji cha Koresa, Kata ya Kirua Vunjo Kusini wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro, wamekubaliana kuchagua viongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwezi ujao nchini watakaobeba ajenda kuu ya kutatua kero ya uhaba wa maji na kudhibiti ukatili kwa wanawake na watoto kwa vipigo.

Msimamo huo wametoa kutokana na kijiji hicho chenye wakazi 5,033, kukosa majisafi na salama ya bomba na kusababisha wanawake na watoto kutumia muda mwingi kusaka huduma hiyo kwa kutembelea umbali mrefu na kujikuta wakiambulia vipigo kutoka kwa waume na baba zao wanaporejea nyumbani.

Walitangaza msimamo wao huo jana wakati wakizungumza jana katika kikao kazi cha wadau wa Mradi wa Sauti ya Haki, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO.

Mmoja wa wakazi hao, Happyson Temba, alisema ili kutokomeza vitendo hivyo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, maji ni ajenda kuu kwa wagombea Grace Mfinanga, alisema uhaba wa maji na kuelemewa usambazaji huduma hiyo katika Mradi wa Jumuiya ya Watumia Maji wa Uchira, kumewafikirisha waamue katika uchaguzi huo utakaofanyika Novemba 27 mwaka huu, kuja na ajenda kuu ya maji maji kwanza. "Sisi wanawake tunaotaka kugombea pamoja na wanaume, tunataka kijiji chetu ajenda mojawapo iwe ni maji kwanza katika mikutano yetu ya kampeni za kujinadi kisiasa ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili," alisema Diwani wa Viti Maalum Mstaafu, Aneth Mfinanga.

Mratibu wa Mradi wa Sauti ya Haki, Veronica Ollomi, alisema pamoja na masuala ya uchaguzi, mradi huo unashughulikia uimarishaji haki za kifeminia na haki za kijamii.

**"Sisi wanawake tunaotaka kugombea pamoja na wanaume, tunataka kijiji chetu ajenda mojawapo iwe ni maji kwanza katika mikutano yetu ya kampeni za kujinadi kisiasa ili kutafuta..."**

Alizitaja kata zinazotekeleza mradi huo kuwa ni Pasua na Ngangamfumuni (Manispaa ya Moshi), Mabogini, Mwika Kusini, Mwika Kaskazini na Kirua Vunjo (Halmashauri ya Wilaya ya Moshi).

"Tunaelekea katika mchakato wa uchaguzi, tumeona tujengeane uwezo. Hatuangalii chama, tunawajengea uwezo watu wote wale wenye nia ya kugombea nafasi za uongozi," alisema mratibu huyo. Mradi huo wa miezi sita, unatekelezwa na KWIECO kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT) kwa lengo la kuendeleza majukwaa ya wanawake kwa ajili ya haki za uongozi kuelekea uchaguzi huo utakaovishirikisha vyama vingi vya siasa nchini.

Ofisa Ufuatiliaji, Tathmini na Taarifa wa KWIECO, Peter Mashingia, aliwataka wanawake na vijana wenye nia ya kugombea uongozi katika uchaguzi huo, kutambua wajibu kuwa mwakilishi wa wananchi ambaye ni kiongozi wa kisiasa, anabeba hatima ya watu wake kwa miaka yote atakayokuwa madarakani.

"Unapotaka kugombea hizi nafasi, hebu waza utatengenezaje mifumo ya kuhakikisha kuna upatikanaji wa fursa mtawalia ili vijana na wanawake waweze kunufaika na hizo fursa; kwa ajili ya kuchakata au kushiriki katika mchakato wote wa uzalishaji na matumizi sahihi ya rasilimali kwa ajili ya maendeleo, kujiimarisha na kuongeza kipato," alisema na kuongeza:

"Hayo mambo lazima uyafikirie vizuri, nyie mnaotaka kugombea au wagombea watarajiwa. Ninyi ambao mmeonyesha nia lazima mwangalie."



Mfamasia wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Benito Ng'ingo, akitoa elimu ya matumizi sahihi ya dawa za moyo kwa wananchi waliofika Arusha Lutheran Medical Centre kwa ajili ya kupata huduma za upimaji na matibabu ya moyo zinazotolewa katika kambi maalumu ya matibabu inayofanyika mkoani Arusha. **PICHA: JKCI**

# Maofisa wajichimbia kutatua migogoro ya ardhi Rombo

**Na Mary Mosha,** ROMBO

VIJIJI 14 wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro vinavyopakana na nchi ya Kenya vimeorodheshwa katika mpango serikali wa kunufaika na matumizi bora ya ardhi.

Timu ya maofisa wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, imepiga kambi wilayani hapa kuwasaidia wananchi kupata thamani ya ardhi yao, kutatua migogoro ya ardhi na kupatiwa hati za umiliki wa rasilimali hiyo.

Akizungumzia mpango huo katika Kijiji cha Keni/Aleni, Ofisa Mwandamizi wa tume hiyo, Buhama Bageni, alisema wameweka kambi wilayani pamoja na mambo mengine kupandisha ardhi thamani.

"Tupo hapa kutambulisha mradi wa matumizi bora ya ardhi, ikiwa ni miongoni mwa vijiji 14 ambavyo vinafanyiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi. Zoezi hili litafanyika kwa vijiji vyote vilivyoko ukanda wa mipakani hasa katika Wilaya ya Rombo.

"Kwa kupanga matumizi hayo, kutawezesha wananchi na serikali kumaliza migogoro baina ya nchi na nchi na kila mmoja ataweza kulinda eneo lake lisingiliwe."

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Mariana Mrina, alisema uhitaji wa wananchi kutaka kupimiwa ardhi yao ni mkubwa, ingawa hawakujua wapi pa kuanzia.

"Kumekuwa kukija mshtaka mbalimbali ya migogoro ya ardhi ofisini kwangu, ambayo inasababisha ndugu kutosalimiana na kutozikana. Mimi na kamati yangu, tumekuwa tukijitahidi kutatua kwa msaada wa ofisa ardhi wa halmashauri, lakini kwa mradi huu, jamii itakuwa na amani na maelewano zaidi," alisema.

Baadhi ya wakazi wa kijiji hicho, akiwamo, Innocencia Mmanda, alisema bado serikali inapaswa kutoa elimu zaidi ili kila mmoja aweze kuelewa.

"Huku kuna migogoro mingi ya ardhi, endapo serikali itatoa elimu kwa gharama nafuu, kila mmoja ataweza kuepukana na migogoro," alisema Mmanda.

Kwa upande wake, Jacob Kimario, aliiomba serikali kuhakikisha zoezi hilo linakuwa endelevu ili kupunguza migogoro ya ardhi.

# Wakulima 'wakitosa' kilimo cha kemikali

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKULIMA wadogo 100 wa mazao ya mboga wa Kijiji cha Masaera kilichoko Kata ya Makuyuni wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro, wameanza kujikita kwenye kilimo ikolojia ili kulinda afya za walaji dhidi ya maradhi ya moyo na saratani.

Ni baada ya kutangaza kuachana na kinachotumia zaidi kemikali za viwandaji kutokana na kubaini kimekuwa kikisababisha madhara kwa walaji mboga na mazao mengine ya chakula.

Wameeleza zaidi kuwa wameelekeza nguvu zaidi kwenye kilimo biashara kwa lengo la kuwanufaisha kiuchumi kupitia matumizi ya mbinu za kisasa na teknolojia bora.

Mtaalamu wa Afya ya Mimea wa Shirika la World Vegetable Center, Dk. Simon Boniface, akizungumza katika shamba darasa la kufundishia teknolojia mpya ya kuvuta na kusukuma wadudu shambani, alisema licha ya kulinda afya za walaji, inasaidia kuongeza mavuno na kuboresha maisha ya wakulima.

Dk. Simon, alisema katika suala la afya ya udongo, kemikali zinaharibu sio tu afya ya viumbe vilivyoko juu ya ardhi na hata vile vya ndani ya ardhi hiyo.

Alisema kuna minyoo muhimu kwenye afya ya ardhi, fangasi na bakteria ambao wanachakata masalia ya mimea ndani ya ardhi na kutoa virutubisho vya kutumika katika mmea.

Mtaalamu wa Kilimo Biashara wa World Vegetable Center, Judith Assenga, alisema teknolojia hiyo imesaidia wakulima kupunguza kiasi cha matumizi ya dawa, hasa za kudhibiti wadudu waharibifu kama vile kimamba na diamond blackmout wa kabichi.

"Wakulima katika kudhibiti hao wadudu wanatumia sana dawa kama vile penetrecer

... afya ya yule anayepiga dawa nayo inakuwa hatarini, na gharama za kupiga ile dawa zinamgharimu sababu ataajiri vibarua shambani ili kupiga dawa," alisema.

Alisema teknolojia hiyo ya kutumia mazao, kuchanganya mazao ambayo yanapungua kiasi cha wadudu shambani, imewasaidia sana kupunguza gharama za vibarua kwa ajili ya kupiga dawa. Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Hamza Mwinyihija, alisema katika teknolojia hiyo, kabichi, kitunguu, mgagani na maharage wanayafanyia majaribio zaidi kwa kuwa ni mahsusi kwa kuvuta wadudu wa kabichi.

...Kwa hiyo teknolojia hii ni nzuri, kwa sababu matumizi ya sumu au viuatilifu imekuwa changamoto kubwa sana, wakulima hawawezi kulima bila ya kutumia sumu. Unakuta sasa zile sumu zinasababisha madhara makubwa sana kama magonjwa ya saratani na Bp (shinikizo la damu)," alisema.

Mkulima, Prosper Tira, Mkazi wa Kijiji cha Masaera, alisema teknolojia hiyo inawasaidia wakulima wa mboga kupunguza matumizi ya sumu kwenye kilimo chao. "Teknolojia hii ikisambazwa kwa wakulima wengine itanufaisha sisi na walaji na kupunguza athari za kemikali kwenye chakula," alisema.

Wakulima hao wanajengewa uwezo kupitia Mradi wa miaka mitatu wa Agroveg, unaotekelezwa World Vegetable Center kwa ufadhili wa Biovision kupitia Taasisi ya ICIPE.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: PROJECT ENGINEER**

**Reports to:** N+1: Maintenance & Inspection Methods EngineerN+ 2: Head of Maintenance & Inspection Engineering

**Job Type:** Full Time - Day time 5d/w - with regular week on duty.

**Location:** Tanga back office with regular travel to EACOP sites (UG&TZ)

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

Project Engineer will be managed by Maintenance & Inspection Methods Engineer at Tanga back - office for the projects, modifications during operation period. Project Engineer will oversee the management of change workflow. She/he will be the focal point for technical study requests and master data updates.

For validated project/modification, She/he will prepare the required scope of work for review & implementation.

The Project Engineer will be expected to travel to remote sites to coordinate project/modification preparation, implementation, commissioning, and hand over.

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

Responsible for coordinating all project elements including engineering, design, quality planning, modifications, installation, commissioning, as well as ensuring the project remains within budget to meet the requirements of the company's needs.

To be responsible for initiation, planning, execution, and closure of Projects or modification.

The Project Engineer must ensure projects are carried out efficiently and on time in co-ordination with the Engineering Maintenance Team and other relevant departments within the EACOP and outside (contractors)

The Project Engineer must work to engineering best practice standards and be compliant with EACOP project specifications.

**MAIN DUTIES:**

- Manages the project within budget.
- Plans project requirements and resources, including the sourcing of subcontract elements, etc.
- Ensures Project /modification request workflow well consider any potential project risks, identifying and establishing corrective actions.
- Assists with design verifications and sign off project progress reports.
- Projects schedule preparation and management to ensure all projects are executed and completed within the planned completion time.
- Undertakes special projects as required and contribute to continuous improvement activities.
- Write project reports and present progress at your supervisor.
- Performs root cause analysis and resolve problems regarding projects.
- Liaises and communicates with other departments, stake holders, suppliers, and other service providers or contractors.
- Complies with the Health, Safety, Environmental and Security (H3SE) Policy prior and during projects execution phase and ensure all project works are executed and completed safely.
- Maintains control of all project documentation.
- Ensures the project's compliance with the applicable codes, practices, policies, performance standards, regulatory requirements, and specifications.
- Participates in all Hazop.
- Preparations of project proposals related to all operational improvement projects.
- Co-ordinates/prepares, implements, and manages any required project related engineering method statements and execution plans.
- Be responsible for the preparation, justification, coordination, implementation, and monitoring of strategic projects, equipment modification and new equipment activities relating to process, utility, facility, and plant equipment as validated by EACOP management.
- Preparation of methods statements for the proposed improvement projects
- Reviews cost estimates, recommendations from vendors, consultants, and licensors.
- Performs overall quality control of the SOW (budget, schedule, plans,) and report regularly on project status.
- Reviews engineering deliverables and initiate appropriate corrective actions.
- Develops and implement project document control procedures, and drafting standards and procedures to organize, store and retrieve documents and information efficiently.
- Ensures a high standard of housekeeping and safe work practices in and around the project areas in general during execution of any project.
- Preparation of TORs and BOQs for procurement of suitable contractors or consultants for the outsourced project works for the procurement of contractors.
- Assists in the preparation of the Annual departmental budget for the project unit.
- Preparation of project reports and prepare periodic or specific reporting of the project activities under his/her responsibilities.
- Manages project and modification workflow.
- Manages EACOP technical master data base (Technical documentation, drawings, 3D models and CMMS)
- Manages engineering service contractor.
- Contributes to HSE performance in line with EACOP objectives.
- Performs any other duties relevant to the scope of work that may be assigned by supervisor.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- BSc. Degree level qualification in an engineering discipline, for example in mechanical, electrical, instrumentation & control, chemical & processing, civil or equivalent qualifications from a recognized institution.
- Master's degree in engineering management (MEM) will be an added advantage.
- Professional Engineer (P. Eng.) registered member with Tanzania Engineers Registration Board (ERB)
- A Project Management Professional (PMP) certified will be highly desired.
- Advanced Microsoft user to include Project and Excel software.
- Proficiency in Oral and written English/Fluency in English, both verbal and written.
- ERB Registration as a Professional Engineer.

**Experience Required:**

- Not less than 5 years of experience in the Oil & Gas industry, major project engineering or a high potential working as project engineer.
- MS office good experience.
- Experience in Microsoft Project and other project management software.
- Strong personality with knowledge in mechanical, Piping, Steel structure Installation & pre commissioning activities for live plants and E&I experience.
- Progress reporting, good communication skills,
- Ability to work with multiple discipline projects.
- Problem solving skills.
- Proven Project Engineering/Project Management experience
- Experience in management of change.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: TELECOMMUNICATION ENGINEER**

**Reports to:** N+1: Head of Maintenance and Inspection, N+ 2: Operation Director

**Job Type:** Full Time - Day time 5d/w - with regular week on duty.

**Location:** Tanga-Back office Frequent travel to EACOP site(s). (1st period expected at Dar es Salaam office)

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

The Telecommunication Engineer will be managed by the Head of Maintenance and Inspection. Telecommunication Engineer will oversee the communication equipment and systems maintenance activities for all EACOP sites. The Telecoms Engineer will be subject to travel to remote sites.

EACOP Telecommunication engineering equipment types are mainly:

- Marine (VHF) Radios and Marine Telecom systems as Berthing Aids system.
- Public Address & General Alarm Systems (PAGA)
- Fiber Optic Communication Network System & Ethernet.
- All telecommunication systems equipment such as computers, system software and hardware & cabling.
- CCTV, PABX, LAN, WAN, VSAT, UHF, VHF, microwave, routers, switches, Intrusion Detection System (IDS) and Ethernet telecommunication systems.

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

**In accordance with policies and procedures in place in EACOP, The Warehouse & Stock Officer is responsible for:**

- Executes/Ensures all Preventive Maintenance (PM), Corrective Maintenances (CM) and major maintenance activities (both planned and unplanned), maintenances of telecommunication system equipment to ensure efficiency and integrity of the telecom equipment.
- Performs modifications and changes required on the telecommunication system to correct all deviations to the allowable ranges (if any).
- Provides a range of services and engineering solutions revolving around different modes of communication and information transfer, such as wireless telephony services, radio and satellite communications, internet, and broadband technologies by ensuring the quality of connections to allow for seamless data and voice transmission are reached.
- Contributes to the development of new telecommunication systems, design or maintenance standards as required using external consultants as required.
- Assists in ensuring the telecom system complies with industry safety, reliability standards and regulatory requirements.
- Contributes to security network obligations related to compliance in relation to all technical requirements, regulations, and legislation certification.
- Conducts Telecom computer diagnostics to investigate and diagnose hardware and software problems.
- Replaces defective components and provide technical assistance/solution.
- Performs data backups and maintain an inventory of communication system equipment spare parts for emergency repairs and normal maintenances.
- Establishes telecom system recovery procedure. regular test or drill to organized as to test the procedure.
- Responsible for understanding and complying with all policies, procedures, and local authorities' regulations relating to the telecommunications.
- Analyzing and testing communication networks for reliability, signal quality, error rate and ranges.
- Completes and submits required frequency coordination forms, Local Regulatory Authority (i.e., Tanzania Communications Regulatory Authority - TCRA) radio frequencies license applications & renewal, and use permits to allow marine radio and microwave communications to take place in accordance with local regulatory authority requirements.
- Prepares radio propagation charts for internal and external client agencies to
- Depict radio coverage on existing or test sites of interest.
- Monitors telecommunications systems to assess the need for updates, upgrades, enhancements, obsolescence, preventive maintenance and/or new systems.
- Performs root cause analysis/troubleshooting and ensure continuous updating of company telecommunication assets and configuration management systems are of high integrity.
- Configures and maintains routers, switches, and hubs for the enterprises' telecommunication network.
- Perform performance fine- tuning and preventive maintenance on network devices, establishing performance thresholds, monitoring performance, and diagnosing and correcting network slowdowns or congestion.
- Prepares RFQ, Technical Bids Evaluation as required. Review the ITB (Invitation to Bid) documents submitted and evaluating and procuring new products and services from vendors.
- Acting as a liaison to telecommunication vendors to maintain critical systems and equipment.
- Work closely to ICT and Instrumentation maintenance engineer during telecommunication system intervention such as fault finding/troubleshooting.
- Ensures a high standard of housekeeping and safe work practices in and around the plant and pipeline facilities.
- Ensures that maintenance activities are performed in strict compliance with COMPANYs current safety rules and operating procedures and in accordance with best industrial practices/standard. Thereby guarantee the quality of the maintenance operations conducted on Site by the Contractor and outside agents.
- Assists in the Preparation of TORs and BOQs for procurement of suitable contractor or consultants for the outsourced maintenance services regarding telecommunication system equipment, works or procurement of goods and spare parts.
- Assists in the preparation of the annual departmental budget for the telecommunication engineering unit.
- Participates in Maintenance Campaign Activities during routine planned or emergency maintenance of campaign zone area and ensure it is done safely and efficiently.
- Preparation of weekly, and monthly maintenance reports and prepare periodic or specific of reporting of the maintenance activities under his/her responsibilities.
- Preparation and updating Standard Operating Procedures (SOP's) for telecommunication systems equipment maintenance and operations.
- Manages sub-contractor for maintenance and inspection of telecom systems.
- Assists in preparation of work pack and end of test report upon completion of job as per client requirement.
- Promotes and implement the company safety, health, and environment policies.
- Contributes to HSE performance in line with EACOP objectives.
- Performs any other duties relevant to the scope of work that may be assigned by supervisor.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- BSc. Degree in Telecommunications engineering/ Electrical Engineering/ Instrumentation & Control Engineering/ Computer Science & ICT or equivalent qualification from a recognized institution.
- Proficiency in Oral and written English.
- ERB Registration as a Professional Engineer.

**Experience Required:**

- Not less than 5 years of experience in Oil & Gas industry, Telecom or a high potential working as Telecommunication engineer.
- MS office good experience.
- CMMS experience/knowledge.
- Experience on plant security systems like Video Access Surveillance System, Access Controls and Identification Management System or Intrusion Detection System (IDS).

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**




Tujitahidi kuondokana na aibu hii

# BUFE

IJUMAA OKTOBA 18, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



**SIRI KUU YA MLIPUKO MAVUNO... Madarasa shambani, mkakati shirikishi unavyotibu parachichi kumea Mufindi**

Ukurasa 12

## AHADI YA RAIS ZIARANI 2022...

# Waziri Mavunde awaanikia hati ujenzi, kiwanda chumvi Kilwa kuanza 2025

• Walianza 1969 kienyeji; sasa kimataifa chini ya STAMICO

**Na Grace Mwakalinga**

MWAKA 2022, wakazi wa Kilwa mkoani Lindi walipopata ugeni wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, walimwasilishia kilio chao mkuu wa nchi, wakihitaji kiwanda cha kuchakata chumvi yao.

Rais akawakubalia kwa kuwaahidi kuwatekelezea. Miaka miwili baadaye, wakawa mashuhuda mnamo Septemba 18 mwaka huu, leo ikitimu mwezi mmoja tangu tukio hilo, wakamwona Waziri wa Madini, Anthony Mavunde akikabidhi hati ya ujenzi wa kiwanda hicho wilayani Kilwa.

"Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye ziara yake katika mkoa huu, moja kati ya mambo aliyoyasikia na kupokea ni kilio cha wazalishaji wa madini ya chumvi na akaagiza kiwanda cha chumvi kijengwe hapa.

"Niwaambie kuwa Rais anafuatilia suala hili la wazalishaji wa chumvi na hatua hii ni utekelezaji wa ahadi yake kwenu baada ya kusikia kilio chenu," anasema Mavunde.

Akafafanua kwamba, hatua waliyoko sasa ni kusimamia maelekezo hayo ya mkuu wa nchi kuhakikisha wanasimamia ujenzi wa kiwanda hicho haraka, ili kutatua kero hiyo ya muda.

Uzalishaji wa chumvi mkoani Lindi, kihistoria ulianza mwaka 1969 na mradi wa ujenzi wa kiwanda hicho sasa, unasimamiwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) katika eneo



Shughuli za uzalishaji chumvi kienyeji Kilwa zikiendelea. **PICHA: MTANDAO**

la Lingaula wilayani Kilwa.

Waziri Mavunde, katika hafla hiyo akaiagiza STAMICO kuhakikisha kabla ya Desemba, mwaka huu ihakikishe wameandaa mafunzo ya namna bora ya kuzalisha chumvi sahihi na yenye ubora unaotakiwa, kuifanya nchi itumie zao la ndani.

Pia, akafafanua kwamba mradi wa kujenga kiwanda hicho unatarajiwa kukamilika ifikapo Aprili mwaka ujao, 2025, hata kuifanya ahadi ya Rais ya mwaka 2022 kwa wakazi wa Kilwa inatimia, kiwanda kikisafisha madini kwa kiwango asilimia 99.5.

Mkuu wa Mkoa Lindi, Zainab Telack, ambaye ndiye alitoa ardhi panapojengwa kiwanda hicho, akasema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kufungua fursa sio tu kwa wakulima wa chumvi, bali wananchi wa mkoa wa Lindi kwa ujumla.

**CHIMBUKO LA UZALISHAJI**

Uzalishaji chumvi mkoani Lindi historia yake ilianza rasmi mwaka 1969, katika lililotajwa wilayani Kilwa, kutokana na kuwa na mazingira mazuri ya uzalishaji wa chumvi mahali hapo pwani ya Bahari ya Hindi.

Hata hivyo, uzalishaji huo kwa muda mrefu, una historia ulianza katika ubora wa chini na ukaendelea kuimarika kadri teknolojia na mbinu za uzalishaji zinavyoboreshwa.

Historia hiyo inafafana na wazalishaji chumvi wilayani Kilwa, wamekuwa wakikabiliana na changamoto za ukosefu wa soko la uhakika, teknolojia duni na bei ndogo za bidhaa yao, wakiwa wanategemea wanunuzi wa kati, ambao mara nyingi hufanya biashara kwa gharama kubwa na chumvi yao haina viwango kimataifa, hali inayoipa thamani ndogo soko.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, anasema kiwanda hicho kitasaidia kusafisha na kuongeza thamani ya chumvi inayozalishwa na wananchi, wenye kilio cha masoko na bei duni.

Wakulima wa chumvi, hasa wa Kilwa wamekuwa wakikabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwamo kukosekana soko la uhakika, teknolojia duni na ubora wa chini wa bidhaa.

Ripoti ya Shirika la Madini ya Taifa STAMICO ya mwaka 2023, inaonyesha uzalishaji chumvi nchini, umekabiliwa na changamoto nyingi, wakulima wengi hawajafanikiwa kufikia ubora unaotakiwa katika masoko kimataifa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wachimba Madini Tanzania, ambaye ni Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Lindi, Palina Ninje, anasema ujenzi wa kiwanda cha chumvi mkoani humo, unawapa fursa wanawake wazalisha chumvi, wanakabiliwa na changamoto za bei duni.

Anataja faida za kiwanda hicho hasa kwa wanawake, ni manufaa ya

Inaendelea Uk 14

## BIASHARA

SIRI KUU YA MLIPUKO MAVUNO...

# Madarasa shambani, mkakati shirikishi unavyotibu parachichi kumea Mufindi

**Na Renatha Msungu aliyekuwa IRINGA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mufindi sasa imejipanga kuhakikisha kilimo cha parachichi, kinazidi kukua kwa kasi zaidi.

Sasa imepanga ina orodha ya mikakati mbalimbali waliojiwekea kama halmashauri, ili kuwainua wakulima wa eneo hilo.

Mojawapo ni kuhakikisha wanashirikiana na taasisi zisizo za kiserikali, ikiwamo Rural Development Organizatiom (RDO) na nyinginezo, kuhakikisha wakulima wanapata uelewa kwenye kilimo wanachokiendesha.

Dira ya halmashauri hiyo ni kuwahakikisha wakulima wake wanaondoka katika kilimo cha mazoea kisichofuata kanuni za maofisa ugani katika maeneo yao, badala yake wahamie kutumia
1. teknolojia.

Mikakati hiyo, imeonyesha kusaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza mavuno ya wakulima wa vikundi, pia mmoja mmoja wanaozalisha parachichi.

Patrick Vavunge, Ofisa Kilimo Mwandamizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, anataja kuwa eneo la kilomita za mraba 6,170, sawa na hekta 617,000, huku kunakofaa kwa kilimo ni hekta 567,640.

Vavunge anasema, parachichi inayolimwa kwa mwaka msimu wa kilimo 2023/2024 ni hekta 1,278, sawa na ekari 3,178, kutoka kwa wakulima wa vikundi na mmoja mmoja wanaolima kibiashara.

Anafafanua zaidi, wakulima parachichi waliotambuliwa na halmashauri hiyo ni 1,351 hadi Machi mwaka huu, kila mwaka wakiongezeka kwenye kilimo hicho.

"Takwimu hizi zinaendelea kupanda mwaka hadi mwaka, kwa sababu wakulima wanazidi kuongezeka kwenye kilimo hicho ambacho hustawi kwa kiasi kikubwa katika halmashauri hiyo," anasema Vavunge.

Anafafanua kuwa, halmashauri Mufundi imekuwa ikiwafunza wakulima namna ya kufuata kanuni, wakishirikiana na taasisi binafsi ya Rural Development Organization (RDO) kuhakikisha kunakuwapo kilimo chenye tija.

Anayataja, mafunzo hayo ni muhimu kutokana na uelimishaji wake kuhusu parachichi, zao wanalolitumia kwa biashara mkoani humo.

Vavunge anasema, halmashauri hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu Bora Tanzania (TOSCI), inatoa mafunzo kwa wakulima na kampuni zinazozalisha mbegu, kuhakikisha wakulima wanatumia mbegu bora ya parachichi.

### KIWANGO MAVUNO

Kuhusu kanuni bora, Vavunge anasema wanaolima kienyeji huvuna kwenye mti mmoja kuanzia parachichi 100, lakini wanaofuata kanuni huvuna kati ya 150 hadi 180.

Pia, anafafanua kwamba wanaotumia teknolojia, kwa mti mmoja huvuna kuanzia parachichi 200. Hiyo ni kutokana na eneo ambalo mkulima amelima.

"Tunajitahidi kutoa elimu ili wakulima wote wafikie idadi ya mavuno ya parachichi 200 kwenye mti mmoja, lengo ni wazidi kuinuka kiuchumi kupitia zao hilo la parachichi," anasema Vavunge.

Anaelezea kuwa uzalishaji kwa mwaka huu umeongezeka, kutoka tani 618.5 za mwaka 2022/23 hadi tani 705 kwa mwaka 2023/2024, na hiyo imetokana na kuwatambua wazalishaji mbegu bora, wanaopata mafunzo kutoka TOSCI, kwa kushirikiana na taasisi nyinginezo.

Anasema taasisi hiyo imekuwa ikitoa mafunzo ya uzalishaji miche bora ya parachichi na mazao menginena wanawapatia vyeti baada ya kuhitimu na wanaendelea kutawanya michezo kwa wakulima.

### MDAU MWANDAMIZI

Mkurugenzi wa Asasi ya RDO, Fidelisi Filipatali, anasema mbali na madarasa ya parachichi, pia wanafunzi wakulima kwa kushirikiana na serikali, vijana wanapata elimu kilimo kwa vitendo.

Anataja fursa wanazotoa zinajumuisha mafunzo kwa vijana wanaochipukia kwenye kilimo, pia wanaungana na serikali kuwekeza kwenye mazao ya bustani.

Filipatali anawataja washirika wao wakuu ni Halmashauri Wilaya ya Mufindi, hasa katika uzalishaji parachichi, vijana nao wakinufaika kupata mafunzo ya zao hilo.

"Ardhi ya Mufindi inakubali mazao mbalimbali, ikiwamo zao hilo. Hivyo, wakulima wanapaswa kujitokeza kulima parachichi kwa sababu soko lake lipo na serikali inasaidia kuwatafutia wakulima masoko ya zao hilo," anasema Filipatali.

Anafafanua Mufindi na halmashauri nyinginezo mkoani Iringa, kunaonyesha ustawi unatokana na maofisa kilimo wake wanawatembelea wakulima na wanawapa elimu na maelekezo ya kitaalamu.

Filipatili anafafanua, siri ya mafanikio katika zao hilo inatokana na wataalamu wa kilimo, wanaotoa maelekezo kwa wakulima kulima kilimo hicho cha biashara mkoani Iringa, lengo ni kukifanya kizoeleke katika ubora wa pekee.

Anasema wanalima parachichi, kupitia maelekezo kutoka kwa wataalamu wanaotoka serikalini, ambao wanawatembelea wanakolima kuwapa elimu na kukagua maendeleo ya shambani.

"Kilimo mkoani hapa kinastawi sana na hii inatokana na wakulima kulima kilimo cha kisasa kwa kufuata maelekezo kutoka kwa wataalam wa kilimo wa sekta hiyo," anasema Filipatali.

### WAKULIMA PARACHICHI

Wakulima wa parachichi, wana maoni kwamba ni kilimo chenye tija, endapo mkulima atafuata kanuni zinazotolewa na wataalamu kabla ya kuanza kuotesha miche na msimu wa mavuno unapowadia.

Josephat Mgimwa, anasema hivi sasa wakulima wengi wanafurahia matunda kujikita katika kilimo hicho, kutokana na kufuata kanuni zinazoelekezwa na maofisa ugani wao katika maeneo yao ya kilimo.

Mgimwa anatoa mtazamo wake kwamba, kilimo hicho kinapoendeshwa kwa ufasaha, kinachangia kwa kiasi kikubwa kuwainua wakulima kiuchumi katika maeneo mbalimbali nchini, akisisitiza haja ya kuwekezwa zaidi, ili kuwainua wakulima.

### MAOFISA KILIMO

Vavunge anasema, changamoto kubwa wanayokutana nayo inajumuisha baadhi ya wakulima wanashindwa kutofautisha magonjwa yanayolikabili zao la parachichi na kukosekana virutubisho lishe kwenye zao hilo.

Anasema, imekuwa kawaida kumtembelea mkulima anayeelezea changamoto ya zao hilo shambani pale, katika ufafanuzi wake anapohojiwa anaangukia majibu ya kuwapo makosa katika uwekaji virutubisho vya zao wakati wa uoteshaji miche.

Kutokana na hilo, anasema maofisa ugani wamekuwa wakiwaelekeza wakulima namna ya kuhudumia parachichi tangu awali, hadi ngazi ya mavuno.



Ofisa Kilimo Mwandamizi wa Wilaya ya Mufindi, Patrick Vavunge (mwenye fulana nyeusi kushoto) na wadau wa kilimo cha parachichi, kwenye shamba darasa lililoko wilayani Mufindi.



Mti wa parachichi ambao mkulima amefuata kanuni za wataalamu wa kilimo. **PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU**

Rai yao sasa wataalamu wa kilimo kwa serikali, ni kwamba itoe mafunzo kwa maofisa ugani ya utunzaji vizuri wa zao la parachichi, kwa sababu katika miaka ya nyuma lilikuwa halilimwi.

Anasema linakuwa zao geni, hata mafunzo kwa maofisa ugani yanatakiwa kila mara, ikiwamo kuhusu magonjwa ya parachichi, yanayopaswa kutolewa kwa maofisa ugani, nao wapeleke ujuzi wanaovuna mafunzoni kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini.

Pia, anaiomba serikali kutoa vibali vya kuajiri maofisa ugani zaidi, kwa sababu waliopo ni wachache, akitumia mfano wachache wa Mufundi wanahudumia vijiji 121 na vitongoji 561.

"Tunaishukuru serikali kwa kuajiri maofisa ugani, lakini tunaomba izidi kutoa vibali vya kuajiri kuongeza ufanisi wa kazi za kila siku kwenye sekta ya kilimo," anasema Vavunge.

Anafafanua kuwa, wataalamu wa mazao ya bustani wako wachache, nako serikali iongeze watu wa sekta hiyo, kukabiliana na changamoto zilizoko katika mazao mbalimbali.

### MIKAKATI YA WATAALAMU

Vavunge anataja mikakati waliojiweka Halmashauri ya Wilaya (Mufindi), inajumuisha kuwaunganisha wakulima kwenye vikundi na kuwatafutia soko, kwa bei elekezi kutoka vyama vya ushirika.

Anataja mingine, ni kuwatambua wakulima parachichi waliopo kwenye vikundi, pia wanaolima kipekee, nao wawakaribishe katika soko la parachichi.


Inatajwa, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, sasa ina mpango wa kujenga nyumba ya kuhifadhia zao hilo, kabla hayajapelekwa kwenye soko la nje.

Vavunge anaishukuru serikali, kwa ushirikiano anayotaja wanaupata kwenye sekta ya kilimo, kitendo kinachochangia sekta hiyo izidi kukua mkoani Iringa.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tujitahidi kuondokana na aibu hii






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

KUNA mwaka fulani walikuja nchini Wazungu wawili; mke na mume wametoka Ulaya. Tuliwashuhudia barabarani tena katikati ya mji wakiwa wote wamevalia sketi!

Tuliwashangaa sana hususan mwanamume ambaye kwetu haijazoeleka. Tuliendelea kuwaangalia kwa mshangao na bahati nzuri walikuwa wakifuatana na mwenyeji wao, Mswahili mwenzetu, ambaye hatukusita kumwuliza kulikoni mwanamume kuvaa sketi kama mwanamke!

Akatujibu ni utamaduni wa kwao. Akasema kwao Scotland, Uingereza, uvaaji huo ni wa heshima sana, hivyo hawaoni tatizo, basi tukaelewa, lakini wakituacha na mshangao wetu, huku tukijisemea nyoyoni kuwa kumbe hata Wazungu ni hamnazo, iweje mwanamume kuvaa kama mwanamke!

Kumbe nikaja kubaini pia, kuwa kuna wakati vijana wetu wa kitanzania, lakini kabila la wafugaji Wamasai, walipata kwenda Ulaya nako wakasababisha mshangao kama hawa Wazungu wa Scotland, kwani wao walivaa lubega!

Hivyo, kumbe utamaduni hutofautiana, kile wewe ukionacho kinakufaa kwa wengine huzua mshangao, lakini ni kutokana na kwamba tuna imani tofauti na kama hazina madhara, basi hapana budi kuzizingatia ili mradi zina mustakabali mwema kwa jamii husika.

Kwa kuwa utamaduni ni imani na mfumo wa maisha ya jamii, hapana budi kukubalika na kutumiwa na jamii yote na hivyo matendo yake hufanana bila kutia chumvi na kuharibu staha ya wengine katika jamii hiyo husika.

Hivi karibuni, nilikuwa nikitazama mtandaoni, ghafla nikamwona kijana mweusi akiwa nadhani Mmarekani, akijinasibu kukanyaga ardhi ya Marekani akitaka kila mtu ajue yuko huko.

Kwa matendo yake, ilikuwa rahisi kila aliyemwona kuamini ilikuwa mara yake ya kwanza.

Awali nilipoona majengo ya Marekani, haraka akili ikanijia kuwa pengine ni Marekani mweusi, kwani alikuwa katikati ya barabara akitamba na kushangilia, mara akirukia magari na kukumbatia watu. Lakini niliposikia lugha ya Kiswahili anaizungumza kwa ufasaha, nikadhani anatoka Mombasa.

Nilipomwonyesha mwenzangu niliyekuwa naye jirani, akasema lafudhi ile ni ya kitanzania na si ya kimombasa. Hivyo nikaamini ametoka Tanzania.

Swali nililobaki nalo kichwani, ni la kwa nini alikuwa akishangilia vile, mara akigalagala barabarani huku Wazungu wakimshangaa na wengine kumpisha.

Akitembea katikati ya barabara kama aliye na changamoto ya afya ya akili, huku magari yakisimama na watu kumshangaa kapatwa na nini kijana yule, akirekodiwa na akimwelekeza mpiga picha wake amfuate kila anakokwenda akiendelea na tambo zake barabarani.

Bila shaka wapita njia waliamini lazima kuna nati ililegea katika sehemu ya kichwa na ndiyo ikimfanya kupagawa vile, huku akijiita sijui balozi wa nini vile, akawa hasikiki vizuri bali makelele na kukumbatia watu akiwaambia: "Umepowaaa! Umepowaaa!"

Jirani yangu akifuatilia kimya kimya picha ile jongefu, ghafla akavunja ukimya na kuniambia "achana na hao machawa tu, hawana lolote, angalia video zingine zenye akili kuliko hao".

Akiniambia siku hizi imekuwa kawaida watu kujifanya hamnazo, ili kupata wafuasi wengi kwenye mitandao.Akasema wengine wanajiita sijui mabalozi wa 'Kazim bey', sijui ndiyo nini, ila kwa kuwa sikutaka anione mshamba, nami nikanyamaza na kujifanya hata hiyo Kazim Bey naijua, lakini kumbe mbumbumbu tu mimi.

Akaniambia wanatumiwa sana na wanasiasa siku hizi, na hivi tunakaribia uchaguzi ndiyo itakuwa balaa.

Nikabaki najiuliza inakuwaje mtu atoke zake Tanzania aende nchi ya watu kufanya fujo barabarani akikumbatia watu asiowajua na kuwashika mikono bila kuelewa utamaduni wao ukoje?

Nasema hivyo, kwa sababu nchi nyingi, mathalan za Mashariki ya Mbali huwa hawashikani mikono wala kukumbatiana wakisalimiana, bali huinamisha vichwa kuonyesha heshima tu.

Sasa kama mtu utatoka huku na kwenda mahali usikojua utamaduni wao na kuwakumbatia eti "umepowaaa" huoni kama unasababisha sintofahamu? Ndiyo sababu katika picha ile jongefu, kijana yule wa kitanzania anakimbiwa au kupishwa na anaotaka kuwakumbatia au kuwashika mikono.

Wahenga walishasema ukienda kwa wenye chongo, nawe vunja lako jicho, ili ufanane nao na ufuate utamaduni wao, kuliko kuwakera na ukichaa wako barabarani na kusababisha taharuki isiyo na lazima.

Kwa maana nyingine starehe zako zisiwe kero kwa wengine. Hata kama tunatafuta wafuasi mitandaoni, basi tufanye kwa kiasi kuliko kuaibisha Taifa letu kwa sifa zisizo na kichwa wala miguu.

Halafu inashangaza awamu hii ndiyo wameibuka machawa wengi wa aina hii wanaotuchefua kwa sifa rahisi rahisi! Tujirudi inawezekana, kwani muda upo bado.

UCHUMI

MIAKA 18 YA MAADHIMISHO

# Siku ya Wanawake Waishio Vijijini na mzigo utamaduni unaowaelemea

**Na Mwandishi Wetu**

JUMANNE wiki hii Oktoba 15, dunia imeadhimisha Siku ya Wanawake Waishio Vijijini, huku ikielezwa kundi hilo linakabiliwa na changamoto lukuki, ikiwamo ukosefu wa elimu, ardhi, fursa za maendeleo, sambamba na kuathiriwa na mila kandamizi.

Wanawake kutoka maeneo tofauti ya vijijini nchini, wanaeleza changamoto wanazopitia kutokana na mazingira yao, akiwamo Aneth Mwinama, mkazi wa Kijiji cha Chikunja, Wilaya ya Masasi, Mtwara, anasema mifumo ya utoaji mikopo kwao walio vijijini haiendani na mazingira yao, hivyo inawanyima fursa.

"Kwa huku vijijini, wengi hatuchukui mikopo kwa sababu tuna kipindi cha kupata hela za mikopo, kwa kipindi cha kufikia Januari hadi mwezi wa Tano. Sisi wa vijijini hali zetu zinakuwa ngumu na biashara inakuwa ngumu.

"Kuanzia mwezi wa sita hadi 12, wengi wetu tunakuwa na hali nzuri, kwa sababu pale tunauza mazao kama mbaazi na ufuta. Biashara zinakuwa zimechangamka," anaeleza Aneth.

Mwaka huu, siku hiyo imepambwa na kaulimbiu: "Wanawake wa vijijini wanaodumisha uoto wa asili, kwa mustakabali wetu wa pamoja, ili kujenga ustahimilivu wa mazingira, kuhifadhi baioanuwai na kutunza ardhi kuelekea usawa wa kijinsia na uwezeshaji."



Mama wa kijijini akipambana na maisha. **PICHA: MTANDAO**

**JAMII YA KIHADZABE**

Katika ufafanuzi wao, kuna maelezo yake Kilimba Kimatingu, Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira, anayefanya kazi kwa karibu na jamii ya Wahadzabe, wilayani Karatu, Mkoa wa Arusha anao ufafanuzi.

Kilimba anasema wanawake wa jamii hiyo wanakabiliwa na changamoto kubwa ya ardhi.

"Wanawake hawa wa Kihadzabe wamekuwa wakipata changamoto ya maeneo yao ya makazi kuuzwa na wanaume wa Kihadzabe. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha uliopita, 2022/2023, kulikuwa na ardhi ya makazi iliyouzwa kwa makabila mengine," anasema Kilimba.

Pia, anaeleza kinamama hao kutokana na mila zao, wanaamini katika kujifungua nyumbani, hali inayochagiza ukosefu wa huduma bora za afya ya uzazi kwa wanawake wa jamii hiyo.

Mkazi wa Kata ya Domanga, Regina Biyo, naye anaeleza changamoto zinazowakabili wanawake katika maeneo yao.

"Kwenye tamaduni zetu, mama ndiye anajenga nyumba, mwanaume hahusiki katika hilo. Kwa hiyo, unakuta kwa asilimia kubwa mama ndiye ahangaike ajenge nyumba, watoto wale wavae, wafanyaje.

"Haya ndiyo maisha yetu, hatulimi, tunategemea matunda na kuchimba mizizi ili watu wale. Inakuwa ngumu, ndiyo maana unakuta mama wa Kihadzabe anazeeka haraka kuliko wanaume."

**MAADHIMISHO YALIKOANZIA**

Siku ya Wanawake Waishio Vijijini ilianzishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) mwaka 2007 chini ya Azimio mambari 62, ili kusherehekea umuhimu wa kundi hilo na kutumia muda huu kutafakari changamoto zao na kuzifanyia kazi.

Wanawake waishio vijijini, wanatajwa kuwa ndiyo uti wa mgongo wa mazao ya kilimo, wakichangia uzalishaji wa chakula na lishe na ndilo kundi linalosimamia ulinzi na usalama wa watoto.

Hata hivyo, licha ya mchango wao, wanawake hao wanakabiliwa na changamoto lukuki hasa ukosefu wa haki ya kutoa maamuzi.

Siku ya Wanawake wa Vijijini, inatoa fursa ya kutambua na kusherehekea mchango wa wanawake hawa katika jamii, ikitajwa ni muhimu kuwapa wanawake wa vijijini fursa za elimu, rasilimali na uongozi ili waweze kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya jamii zao.

Hiyo itachangia si tu katika kuboresha hali zao, bali pia katika kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla.

Kwa hivyo, inasisitizwa ni wajibu wa kila mmoja kuunga mkono juhudi za kuhakikisha wanawake wa vijijini wanapata haki na fursa zinazostahili.

• *Kwa mujibu wa DW*

## WAZIRI MAVUNDE AWAANIKIA HATI UJENZI, KIWANDA CHUMVI KILWA KUANZA 2025

Inatoka Uk 11

soko, bei nzuri ya bidhaa yao, hivyo kuwaongezea kipato, sambamba na kupata mafunzo ya kuongezea thamani bidhaa yao.

"Tutanufaika si tu katika uzalishaji wa chumvi yenye viwango vya kimataifa, bali pia kuwapa uwezo wa kushiriki katika masoko ya kimataifa, kwa kuimarisha ushirikiano kati ya serikali, taasisi za kifedha na wakulima.

"Uwekezaji huu unatarajiwa kuboresha maisha ya wanawake na kuhamasisha ukuaji wa uchumi katika jamii zao," anasema Ninje.

Waziri Mavunde ana ufafanuzi wa ziada: "Serikali pia inakusudia kushirikiana na taasisi za kifedha, ili kuwasaidia wakulima kupata mikopo nafuu kwa ajili ya kuwekeza zaidi katika shughuli zao za uzalishaji wa chumvi. Hatua hizi zote zinalenga kuboresha sekta ya chumvi nchini na kuleta mafanikio kwa wakulima wadogo."

**NGUVU YA SOKO**

Kiwanda hicho cha kusafisha chumvi kitakapokamilika, kinatarajiwa kunufaisha wazalishaji kupata bei nzuri ya bidhaa zao, huku wakishiriki katika masoko kimataifa.

Mkurugenzi wa STAMICO, Dk. Vennance Mwasse, anasema kiwanda hicho kitakapokamilika Aprili mwaka ujao, kitaweza kuzalisha tani 200,000 za chumvi kwa mwaka.

Anasema, ni hatua itakayoongeza uzalishaji chumvi nchini na kusaidia kupunguza utegemezi, pia uagizaji kutoka nje.

Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaonyesha mahitaji ya chumvi safi na ubora kimataifa, yanaongezeka kwa kasi katika masoko kimataifa, hususan Mashariki ya Kati, Ulaya na baadhi ya nchi za Asia.

Hapo kuna ushauri kitaalamu, wazalishaji chumvi nchini Tanzania, wanaweza kunufaika na soko hilo kwa kutumia kiwanda hicho cha kisasa.

Serikali imekuwa ikielekeza imepanga kuwekeza katika teknolojia za kisasa za kusafisha chumvi, zitazosaidia kuongeza uzalishaji wa chumvi yenye ubora wa kimataifa.

**TAASISI FEDHA, WAKULIMA**

Ili kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kwa mafanikio, ushirikiano kati ya serikali, taasisi za kifedha na wakulima ni muhimu, STAMICO ikiwa na jukumu la kusimamia ujenzi wa kiwanda na kutoa mafunzo kwa wakulima.

Mkuu wa Mkoa Lindi, Zainab Telack, anasema wanawajibika kuhakikisha mazingira bora ya utekelezaji mradi huo na kuondoa vikwazo vyote vinavyoweza kujitokeza.

Anasema wakulima wana jukumu la kushiriki kwenye mafunzo ili waboresha chumvi wanayozalisha, wakielewa ujenzi wa kiwanda hicho unategemea ushirikiano wao katika mbinu mpya za uzalishaji.

**CHANGAMOTO/ SHERIA**

Inaangaliwa kitaalamu, kuna changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wake, ikiwamo kufikia viwango bora vya kimataifa sokoni.

Kuna mtazamo katika namna upatikanaji wa rasilimali zinazokidhi mahitaji kuendesha kiwanda hicho katika viwango vinavyohitajika, pamoja na kusimamia vizuri ushirikiano kati ya wakulima, serikali na wawekezaji.

Ujenzi wa kiwanda hiki unaendana na sheria, pia kanuni zinazolenga kulinda na kuimarisha sekta ya uzalishaji chumvi nchini, ikiwamo Sheria ya Madini, inayomamia rasilimali za madini, ikiwamo chumvi.

Sheria hiyo inaweka taratibu za upatikanaji wa leseni za uchimbaji na uzalishaji wa madini, pamoja na masharti ya mazingira yanayohitajika katika shughuli hizo.

Aidha, Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, inalenga kulinda mazingira katika shughuli za uzalishaji wa madini, hivyo kiwanda tarajiwa kiangukia katika kufuata masharti yaliyowekwa katika sheria hiyo, kuhakikisha uzalishaji chumvi hauharibu mazingira ya eneo hilo.

Sheria ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda nchini Tanzania ya Mwaka 2009, inalenga kuimarisha shughuli za utafiti na maendeleo katika sekta ya viwanda, ili kuchangia katika maendeleo ya uchumi kitaifa.

Hapo inasimamia masuala kama vile utafiti wa kiteknolojia, ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi na uwekezaji katika maendeleo ya viwanda. Ni sheria inayosaidia kuweka mazingira mazuri kwa uvumbuzi na matumizi ya teknolojia mpya katika uzalishaji wa viwanda.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: MAINTENANCE COORDINATOR**

**Job Type:** Full Time – and duty period to consider.

**Reports to:** N+1: Maintenance Superintendent, N+ 2: Head of Maintenance and Inspection

**Location:** MST – Tanga regular travel to EACOP site to consider.

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

- As Maintenance Coordinator, you will manage and optimize the maintenance planning for all perimeters.
- Perimeters are: PS1 perimeter, PS4 perimeter, PS5 perimeter and MST perimeters.
- You will follow interface with loading operation and upstream feeders.
- You will interface with all maintenance disciplines, logistics and others EACOP activities to optimize maintenance execution without impacting.
- This means you will be able to shape and develop a central role with great influence in safe, timely and effective execution of preparation and coordination of activities. This is with the possibility to continuously use and develop your competencies in ensuring the quality and effectiveness of planned activities.
- You will manage maintenance opportunity activity portfolio and coordination process.
- You will get to use your knowledge and experience applying a range of techniques to support fabrication and campaign engineer.
- You will adapt maintenance planning to EACOP constraint, site accessibility, and seasonal weather conditions.
- You will manage and review procedure and workflow related directly and or indirectly to maintenance coordination.

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

- Contributes to HSE performance in line with EACOP objectives.
- Integrates into an execution plan the "campaign-able" activities prepared by Maintenance, Inspection Services, Engineering & Construction
- Ensures the Work Packs, Procedures, logistics, Permits to Works, Risk Assessments and Toolbox Talks are well integrated in maintenance planning.
- Ensures the main resources of the scopes are provided in time by the Support Entities
- Communicates to the maintenance disciplines any update who may impact planned activities.
- Manages maintenance coordination meetings.
- Participates in operation planning meetings.
- Manages interface and coordination tools.
- Analyzes planned past activities to improve coordinatization needs.
- Manages coordination processes and workflows.
- Contributes to the 2-Year visions of planned campaigns and the 90-day planning.
- Influences the 90-day planning.
- Influences the 5-week planning.
- Issues T-REX.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- Bachelor level or similar
- Proficiency in oral and written English
- Good knowledge of CMIMS (Computerized Maintenance & Inspection Management System).
- Planning software and IT workflow tools knowledge.
- ERB Registration as a Professional Engineer

**Experience Required:**

- 4-6 years of experience in Oil & Gas industry or a high potential
- Site -multi sites and multidiscipline planning preparation or activity management experience.
- Maintenance Contract management.
- Full field/Industrial site shut down experience.
- Primavera or similar good experience.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: MECHANICAL (ROTATING) ENGINEER**

**Job Type:** Full Time, 5 d/w and subject to regular duty weeks

**Reports to:** N+1: Head of Maintenance and InspectionN+ 2: Field Operations Manager

**Location:** Tanga (primary location during readiness preparation will be Dar es Salaam) - regular visits to EACOP sites.

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

As Mechanical Rotating Engineer for EACOP, he / she will manage, report and support mechanical activities in 4 perimeters.

**Main rotating equipment of assets are:**

- 18 export pumps variable speed: 3500 KW each.
- 3 export loading pumps.
- 19 Diesel/ Crude Generator packages: Caterpillar 3616.
- 10 Emergency diesel generators.
- 12 Fire water pumps.

**Support to Site Mechanical Technicians:**

- 9 Site Technicians.
- 1 Maintenance Engineer for (PS1-Perimeters (Uganda)

**Service Maintenance Contracts:**

- Pump Packages.
- Genset Packages.
- Local mechanical repair workshops.
- Loading Arms.
- Lubricants.

- Objectives will be defined in operation as to optimize asset availability, operating cost, and asset efficiency.
- The job holder is the focal point for all EACOP's rotating equipment. He / she will Interface regarding activity planification and with other entities.
- The job holder is also accountable for demonstrating individually exemplary behavior towards HSSE rules & requirements, and for ensuring their application within his scope of responsibility.
- The job holder reports to the Maintenance Leader.
- This means you will be able to shape and develop a central role with great influence in safe, timely and effective execution of mechanical maintenance activities. This is with the possibility to continuously use and develop your competencies in ensuring the quality and effectiveness of mechanical maintenance activity reporting, sub-contractor efficiency and work preparation for future major maintenance.

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

- Monitors rotating equipment according to maintenance philosophy and will manage dedicated Specific Maintenance Contracts (SMC).
- Verifies contractual parameters and performance standards of mechanical equipment complying to allow Project handover to Operations.
- Provides Mechanical support to cover the obligations in terms of maintenance strategy update, performance monitoring, contract, and stock strategy. Define priorities to focus on delivering values matching with Field Operations Objectives.
- Prepares and follow major rotating equipment major maintenance.
- Main equipment availability and reliability monitoring: Ensure the management system is up to date and in line with the Area performance objectives. Recover any REX from Area and analyze KPI to set-up maintenance strategy accordingly.
- Assess and audit procedure managing material repair in workshop are well implemented to secure reliable tracking system, follow-up, and progress.
- Ensures stock management by technology in line with criticality study, capability to repair and availability objective.
- Optimization: Review and challenge maintenance plan on rotating equipment's and do proposal to reduce downtime and cost to optimize cost VS running hours.
- Secures life cycle management of equipment's/ packages; implement studies and action plan to secure maintainability of the plants (obsolescence).
- Develops periodic reporting activities and follows them.
- Advise for the diagnosis related to major malfunctions and failures. Comments Contractor action plan and assess site competencies and process to solve major malfunctions and failures. Support site if required.
- Organizes and maintains mechanical equipment's database. Guarantee the quality of activity reporting, particularly though CMMS.
- Establishes Maintenance Contractors performance indicators, related to Discipline, according to FO objectives and regularly evaluate their performance.
- Ensures condition monitoring philosophy is efficient and develop required tools.
- Proposes improvements to the maintenance strategy according to Site needs.
- Contributes, under the Service perimeter of responsibility, for the integration of future developments of EACOP.
- Defines, lead / supervise the Discipline studies needed to achieve the objectives in terms of availability, maintainability, and equipment operating cost. Elaborate (approve) for the Discipline, the functional specifications related to process modifications.
- Receives studies / developments / equipment for Discipline.
- Follow Long Lead items required for the execution of the AREA work program are provided on time by the technical support.
- Reviews CONTRACTOR Contract strategy and develops scope of work, accordingly, assist to technical clarification organized by contract support; assist contract engineer in the different tendering stage where technical administrator is required.
- Reports Contractors' Maintenance performance. Propose improvement to evaluate feasibility to implement them.
- Assist Cost control in the different NON-ROUTINE Invoice validation stage where technical administrator is required.
- Works closely with CONTRACTOR Maintenance team to provide supply and services in his area of responsibility.
- Contributes to the improvement of skills and know-how.
- Evaluate personnel. Participate in interviewing employees and provide feedback for mechanical technicians.
- Participates and updates REX and recommendation for future contract as EACOP strategy.
- Contributes to the 2-Year visions of planned campaigns and the 90-day planning.
- Influences the 90-day planning.
- Influences the 5-week planning.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- Engineering Bac +5 level with specialization in Mechanical Rotating Machines, or equivalent proven experience (Engineer)
- Languages: English proficiency
- ERB Registration as a Professional Engineer

**Experience Required:**

- Experience in Rotating Machinery (over 8 years), competence in vibration analysis, oil production knowledge.
- Experience in industrial maintenance (over 5 years) and maintenance methods (RCM monitoring machines and CMMS use)
- Experience of maintenance team and contractor management.
- Reliability, autonomy, analytical, organizational capacity, and leadership.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: METERING ENGINEER**

**Reports to:** N+1: Instrument and Control Engineer
N+ 2: Head of Maintenance and Inspection

**Job Type:** Full Time - Day time 5d/w - with regular week on duty

**Location:** MST and frequent travel to PS1 and PS4/5

**WHO WE ARE**

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

**JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION**

- Metering Engineer will be managed by Instrument and Control Engineer for MST-Tanga (back office). The Metering Engineer will oversee the metering maintenance activities at PS1, MST, PS 4 & 5. She/he will provide support for metering to PS1 instrument engineer. She/he will be the focal point for metering technical interfaces with feeders, partners, and authorities.
- The Metering Engineer will be subject to frequent travel, mainly PS1.
- She/he is responsible for the maintenances of all flow meters and contract services required for metering systems.

**EACOP Metering engineer equipment types are mainly:**

- Export Flowmeters and other related metering control systems.
- Feeder metering packages at PS1.
- PS4, 5 and MST metering package for CRO Genset.
- All metering and measuring instruments as proof loop system.

**DUTIES & RESPONSIBILITIES**

- Ensures flowmeter maintenance properly done or carry out flow meters maintenance activities, both planned preventive and corrective as planned by maintenance system – CMMS for all flow meters and related systems.
- Performs breakdown repairs of flow meters, metering system and measuring instruments whenever required and be pro-active in identifying opportunities to improve integration, accuracy, equipment reliability and performance.
- Carries out fault-finding (troubleshooting) and diagnosis of problems affecting crude oil metering system and take corrective action/measures to anticipate and prevent downtime and thus maximize productivity and production availability.
- Responds as appropriate to plant upsets and emergencies.
- Ensures a high standard of housekeeping and safe work practices in and around the plant and facilities.
- Ensures that maintenance activities are performed in strict compliance with COMPANYs current safety rules and operating procedures and in accordance with best industrial practices/standard. Thereby guarantee the quality of the maintenance operations conducted on Site by the Contractor and outside agents.
- Assists in the installation of modifications and new metering equipment.
- Assists in the Preparation of TORs and BOQs for procurement of suitable contractor or consultants for the outsourced maintenance services regarding flow meters and meters, works or procurement of goods and spare parts.
- Assists in the preparation of the annual departmental budget for the metering unit.
- Preparation of maintenance reports and prepare periodic or specific of reporting of the maintenance activities under his/her responsibilities.
- Participates in all aspects of EACOP Pipeline Metering Operations
- Ensures usage of Valid Metering Calibration Equipment having an accuracy better than or at least equivalent to the reference accuracy of the instruments calibrated by planning, supervising, and ensuring all flow meter's calibrations are performed by a competency and certified contractor in accordance with the manufacturers and operations recommended specifications.
- Maintains all the fiscal metering systems to ensure the integrate and accuracy and ensure the measured quantities and allocated volumes are accurate and comply with the standards and local regulation.
- Coordinates with EACOP customers and performs all aspects of the Crude oil measurement both for transmission systems to the MST export metering station.
- Provides assistance during any Metering System rectification/modification or upset and perform Metering System Validation and Certification on pipeline system.
- Ensures and oversees the usage of Valid Metering Calibration Test Equipment having an accuracy better than or at least equivalent to the reference accuracy of the instruments calibrated.
- Preparation and updating Standard Operating Procedures (SOP's) for flow meters and meters related systems operations and maintenance.
- Works closely with Instrumentation and Control Maintenance Engineer, provide/clarify flow rate equation formulae to be entered and used on the DCS and when required, assist the Process Engineer in carrying out monitoring of flow meters and metering system.
- Advises the laboratory personnel on the possible sources of uncertainties in laboratory methods of fluid measurement and proposes means of improvement.
- Assures the integrity of all flow meters, test equipment and rectify if there are any deviations.
- Interface and coordinate with the flow meters vendors and calibration contractors for calibration and outsourced flow maters maintenance/calibration services to ensure the flow meters reliability and accuracy during (operations) measurements process.
- Reviews and manages maintenance plan, spare inventory and all other related administrative tools in the systems as regards metering maintenance on site.
- Assists in preparation of work packs and end of test reports upon completion of jobs.
- Promotes and implements the company safety, health, and environment policies.
- Contributes to HSE performance in line with EACOP objectives.
- Performs any other duties relevant to the scope of work that may be assigned by his/her supervisor.

**HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES**

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

**QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED**

**Academic Qualifications:**

- BSc. Degree in Electrical/Instrumentation/Electronics or equivalent qualification from a recognized institution.
- Short course certificates (vendor or regulatory authority) in Flow Measuring and Metering Equipment/instrument Maintenances will be an added advantage.
- Proficiency in oral and written English.
- ERB Registration as a Professional Engineer.

**Experience Required:**

- Not less than 5 years of experience in the Oil & Gas industry or a high potential working as a metering engineer in other industries.
- MS office good experience.

**HOW TO APPLY**

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is on 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

# Watoto wenye mtindio ubongo wapelekwa kwa sangoma

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO 17 kati ya 1,000 wanaozaliwa nchini wana mtindio wa ubongo na kuathiri ukuaji wao na wengine kupata ulemavu wa kudumu kutokana na wazazi kuwapeleka kwa waganga wa kienyeji kwa imani za kishirikina.

Vilevile, imeelezwa baadhi ya watoto hao wanachelewa kupatiwa matibabu kutokana na wazazi wao kuhusisha hali hiyo na imani za ushirikina na kuwalazimu kuwapeleka kwa waganga hao maarufu kwa jina la sangoma.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Vijiji nchini, Dk. Benard Mbwele aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa tiba ya mazoezi kwa watoto hao katika Wilaya ya Mbeya.

Dk. Mbwele, alisema wameanzisha huduma hiyo kusaidia watoto hao kuimarisha viungo vyao na kuwa na uwezo wa kufanya shughuli mbalimbali, ikiwamo wa kuandika.

Alisema wazazi wenye watoto wenye matatizo hayo wanatakiwa kuwapeleka hospitalini badala ya kwa waganga hao kupata matibabu.

"Tunalenga kuwasaidia watoto hawa ili wawe na uwezo wa kumudu baadhi ya shughuli zao, wale ambao walikuwa wanaonekana hawawezi kuandika wataandika na hata kucheza watacheza," alisema Mbwele.

Mtaalamu wa Mazoezi ya Viungo wa Taasisi ya Agarimo For Africa, Dk. Ledicia Fernandes, alisema walifanya utafiti mwaka 2021 na kubaini Mbeya ina idadi kubwa la watoto wenye mtindio wa ubongo.

Fernandes, alisema waligundua hakuna mpango wa kuwasaidia watoto hao kupata matibabu ya mazoezi ya viungo, hivyo kuanza mchakato huo wa kuwasaidia.

"Tuliamua kuanzisha mpango huu ili kuwasaidia watoto hawa, sisi tunalenga kuwasaidia watoto hawa kuimarisha viungo vyao kwa kuwafanyisha mazoezi ya viungo," alisema Dk. Ledicia.

Katibu wa Hospitali ya Ifis, Fausitina Mahenge, alisema wameanzisha huduma hiyo kuwasaidia watoto hao hasa wakiwa wadogo ili kuchangamsha ubongo.

Alisema wameweka vifaa vya kisasa na wataendelea kufunga vingine ili kukidhi mahitaji yao.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Khamis Ally, alisema mahitaji ya matibabu ya viungo kwa watoto yanahitajika kwa kiasi kikubwa katika wilaya hiyo kwa kuwa ina idadi kubwa ya wenye tatizo hilo.

Dk. Ally, aliwaomba wadau kushirikiana na serikali kuwasaidia watoto hao ili wafikie ndoto zao na kuwapunguzia wazazi gharama za matibabu.

# Barabara Isyonje - Makete hatarini kukatika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATUMIAJI wa Barabara ya Isyonje-Makete inayounganisha mikoa ya Mbeya na Njombe wamekumbwa na hofu ya kukatika kwa mawasiliano mvua zitakapoanza kunyesha kutokana na kutofanyiwa ukarabati.

Watumiaji hao wamedai kuwa barabara hiyo ina makorongo yaliyosababishwa na maji ya mvua za msimu uliopita, hivyo kuhatarisha usalama wao na vyombo wanavyotumia kusafiria.

Wakizungumza na Nipashe juzi, waliomba serikali kuifanyia ukarabati barabara hiyo kabla msimu ujao wa mvua haujaanza ili kuinusuru kukata na kukosekana kwa mawasiliano baina ya mikoa ya Mbeya na Njombe.

Mmoja wa watumiaji hao, Sinai Mwasanga, alisema maisha ya wajawazito yako hatarini wakati wa kwenda kujifungua kwenye vituo vya afya vilivyoko Mbeya Mjini kwa kuchelewa kufika kwa wakati.

Mwasanga, alisema hivi karibuni mjamzito alijifungua watoto pacha, mmoja njiani baada ya kushindwa kufika hospitalini kwa wakati na mwingine Hospitali ya Igawilo.

"Barabara yetu ni mbovu na inatusababishia matatizo, wanawake tunapokwenda hospitalini tunashindwa kufika kwenye vituo vya afya kwa wakati, tunaomba serikali itusaidie kuboresha barabara hii ili tuokoe maisha yetu," alisema Sinai.

Alisema yeye anaishi Kijiji cha Ilungu ambako huduma za afya bado kuboreshwa na kwamba serikali iliwaahidi ingepeleka gari ya kubeba wagonjwa bila mafanikio.

Mzee Leonard Mwanyonga, alisema kulingana na hali ya hewa ya eneo hilo kuwa na mvua nyingi, barabara zinatakiwa kukarabatiwa wakati wa kiangazi.

Alisema barabara hiyo ikikarabatiwa wakati wa mvua inageuka tope na kushindwa kupitika.

"Kuna watu wanaishi Isyonje lakini wanalima Kikondo sasa mvua ikinyesha hawawezi kusafirisha mazao yao kwa sababu barabara hii inaweza ikakatika muda wowote, wakija kuikarabati wakati wa mvua inanyesha wataharibu zaidi," alionya Mwanyonga.

Alisema wamiliki wa magari ya kubeba mazao huwa wanawatoza fedha nyingi za kusafirisha mazao yao wakidai wanafidia gharama za matengenezo ya magari yao baada ya kuharibika.

Mmoja wa madereva wa magari yanayosafirisha viazi kutoka Kikondo, Vedasto Nyambo, alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo, magari yao yamekuwa yakiharibika mara kwa mara na kupata hasara.

Alisema ikitokea gari kubwa limekwama kwenye barabara hiyo wanalazimika kusubiri mpaka litengenezwe na kuendelea na safari.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema barabara hiyo ni miongoni mwa barabara ambazo zimeainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kujengwa kwa kiwango cha lami.

Homera, alisema ujenzi wa barabara hiyo ulianzia Wilaya ya Makete mkoani Njombe na kwa sasa wanasubiri fedha zipatikane ili mkandarasi mwingine aanzie Isyonje kuelekea Makete.

Aliwataka wakazi wa maeneo yanayopitiwa na barabara hiyo kuendelea kuwa wavumilivu wakati serikali inaendelea na mikakati ya kuijenga.



# Mikopo ‘kausha damu’ inavyosababisha msongo wa mawazo wilayani Muheza

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa**
MUHEZA

MIKOPO ya kausha damu imelalamikiwa na wananchi kutokana na riba kubwa na kusababisha baadhi ya wakopaji kupata msongo wa mawazo na wengine kuhama makazi kwa kukimbia kulipa madeni.

Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, umekuwa mkombozi kwa baadhi ya wananchi hasa wakulima wa viungo katika Tarafa ya Amani, wilayani Muheza, mkoani Tanga, kwa kuwapa elimu ya kuweka na kukopeshana wenyewe bila kuweka dhamana ya mazao yao kabla ya msimu wa mavuno.

Wakitoa ushuhuda kwa waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), wilayani humo kwa ajili ya ziara maalumu ya mafunzo ya kuangalia miradi ya maendeleo, walisema mikopo ya kausha damu inawanyima uhuru na muda wote huwaza jinsi ya kulipa deni hilo huku baadhi yao wakikimbia kwa kuhama makazi yao na kwenda kusikojulikana.

Emmanuel Chamungwana ambaye ni miongoni mwa wananchi wa kijiji cha Kwezitu, alisema mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, umewaondoa kwenye mikopo ya kausha damu kwa kuwapa elimu ya kuweka na kukopeshana wenyewe bila kuweka dhamana ya mazao yao kabla ya msimu.

Alisema kabla ya mradi huo, wenye mikopo walikuwa wakiwapa masharti magumu, ambayo yalikuwa ni mateso, lakini ujio wa USAID Tuhifadhi Maliasili umewasaidia kuondokana na mikopo ya kausha damu.

Mwenyekiti wa MJUMITA, Esther Mzalia, alitaka serikali kuangalia namna ya kuwafikishia mikopo nafuu wakulima hasa vijijini ambao wengi wao maisha yao ni duni.

Mtendaji wa Kata ya Kwezitu Esther Kilua, alisema ujio wa miradi mbalimbali ya maendeleo ukiwamo wa USAID Tuhifadhi Maliasili umewasaidia wakulima kujitambua na kuiona thamani ya kilimo.

Kuhusu ombi la serikali kutoa mikopo kwa wakulima, Kilua alisema tayari imeshatoa nafasi hiyo na watu walio kwenye vikundi wameshaanza kukopeshwa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwezitu, Christopher Kallaghe, alisema, pia USAID imesaidia kuwapangia kijiji chao kwenye mpango wa matumizi ya ardhi.

Kallaghe alisema, mpango wa matumizi ya ardhi umewasaidia kuondokana na migogoro ambayo ilikuwa ikiwatesa kwa miaka mingi kijijini hapo.

Joseph Mkufya mkazi wa Kijiji cha Kwezitu, alisema ujio wa mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili na mradi wa kilimo hai kupitia Shirika la GFP, umewasaidia kuongeza kiwango cha uvunaji wa mazao yao hasa pilipili manga, mdalasini, hiliki na karafuu na wamepewa miche pamoja na kufundishwa namna sahihi ya kulima kilimo hai.

Mtendaji wa Kata ya Kwezitu, Esther Kilua, alisema ujio wa miradi mbalimbali ya maendeleo ukiwamo wa USAID Tuhifadhi Maliasili umewasaidia wakulima kujitambua na kuiona thamani ya kilimo.

Naye Ofisa Maliasili wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Issa Msumari, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wake imekuwa ikijitahidi kutoa elimu kwa wakulima kuachana na mikopo ya kausha damu, kwa sababu ni mateso kwa wakulima.

Msumari alisema, serikali inatoa mikopo na haina masharti yoyote zaidi inahitaji nidhamu katika kuirejesha mikopo hiyo, na imeshafika kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Muheza.

Aliwataka wakulima waondokane na mikopo isiyo na tija na wajiunge na vikundi mbalimbali vya kuweka na kukopa vyenye masharti nafuu na kuchangamkia fursa za mikopo ya serikali inapowafikia.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa mitambo ya uzalishaji wa hewa tiba (Oxygen Plants) uliofanyika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mjini Magharibi jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali kuendelea kugawa boti kila mkoa Unguja, Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema inalenga kuendeleza zoezi la ugawaji wa boti za uvuvi kwa kila Mkoa wa Unguja na Pemba ili kuisaidia jamii kujiwezesha kiuchumi.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shaaban Ali Othman, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa kampeni ya awamu ya pili ya Mkono kwa Mkono yenye lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Alisema jumla ya boti 10 zitatolewa na kila Mkoa utapatiwa boti mbili ikiwamo ya uvuvi na ukulima wa mwani kuisaidia jamii kujikwamua na hali ngumu ya maisha.

Aliwataka wadau mbalimbali na wenye dhamana kutoa uelewa kwa wananchi kuhusu fursa za kiuchumi zilizoko nchini ili wapate uelewa na kuzifanyia kazi.

Mkurugenzi wa Wakala wa Uwezeshaji wa Wananchi, kiuchumi (ZEEA), Juma Burhani, alisema taasisi hiyo kwa kushirikiana na vyuo vikuu inatarajia kuwawezesha vijana 20 kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali ili kuwainua kiuchumi kujiajiri na kuajiri wengine.

Alisema kupitia kampeni hiyo wanategemea kuvipitia na kuvitambua viwanda mbalimbali vya Unguja na Pemba na kuwashajihisha wananchi kuvitumia viwanda hivyo.

“Mkono kwa Mkono wa msimu uliopita imewasaidia wananchi kupata mikopo baada ya kueleza changamoto zao,” alisema Mkurugenzi Burhan.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Mkurugenzi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Salum Ramadhan na Ramadhan Bukini, walisema wataendelea kutoa taarifa na kuzisambaza kwa wananchi ili kuelewa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kampeni hiyo ya Mkono kwa Mkono awamu ya pili inatarajiwa kuanza Oktoba 19, mwaka huu Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja.

# Mitambo uzalishaji hewa tiba kuondoa usumbufu

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema mitambo ya uzalishaji wa hewa tiba (Oxygen Plants) katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Lumumba itaondoa kadhia na usumbufu wa utoaji wa huduma kwa wagonjwa katika hospitali zote za serikali na binafsi nchini.

Aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa mitambo ya kuzalisha hewa tiba (Oxygen Plants) katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Lumumba visiwani hapa.

Alisema hatua ya kufungwa mitambo hiyo itarahisisha utoaji wa huduma kwa wagonjwa na kupunguza gharama ya ununuzi na usafirishaji wa hewa tiba hiyo ambayo ilikuwa ni kikwazo kikubwa kwa wagonjwa.

Alisema huduma ya hewa tiba itakayozalishwa hospitalini hapo itasambazwa katika hospitali mbalimbali za serikali na binafsi ili wananchi wapate matibabu bora na ya kisasa na kufikia malengo ya serikali ya kutoa huduma zilizobora kwa wananchi wote wa Zanzibar kuanzia ngazi ya wilaya hadi taifa.

Aidha, alisema serikali inafanya juhudi kuhakikisha sekta ya afya inakuwa na madaktari bingwa na vifaa vya kisasa vya kutolea matibabu bora kwa wananchi jambo linaloakisi dira ya maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050 inayolenga kudumisha mfumo wa upatikanaji wa huduma za afya zenye wataalamu bingwa, teknolojia na vifaa vya kisasa vya utabibu.

Hemed alisema, serikali kupitia Wizara ya Afya itaendelea kuweka mazingira bora ya utoaji wa huduma ikiwamo kuifanyia ukarabati Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, kuendelea na ujenzi wa vituo vya afya, kuimarisha upatikanaji wa vifaa tiba na kukamilisha ujenzi wa nyumba za wafanyakazi wa sekta ya afya ili kukaa karibu na sehemu zao za kazi.

Aliwataka watendaji wa Wizara ya Afya ambao watakuwa na jukumu la kuiendesha mitambo hiyo kuitunza na kuifanyia matengenezo kwa wakati na kuitumia kwa uangalifu kulingana na maelekezo sahihi ya utumiaji wa mitambo hiyo.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kuzinduliwa kwa mitambo hiyo kutasaidia kupunguza gharama za ununuzi na usafirishaji wa hewa ya Oxygen pamoja na kupunguza tatizo la kukosekana kwa huduma hiyo.

Mazrui alisema upatikanaji wa hewa tiba hiyo utaamsha ari, kasi na nguvu ya ufanyaji kazi kwa wahudumu wa Afya katika kutoa huduma bora kwa wagonjwa sambamba na kuwashukuru wafadhili na wasimamizi wote waliosaidia kufanikisha kufungwa kwa mitambo hio wakiwamo wafadhili wakuu Global Fund kwa kutoa ushirikiano uliopelekea kukamilika kwa wakati ufungaji wa mitambo hiyo.

Mwakilishi kutoka Gobal Fund, Sara Asimwe, ameshukuru kwa kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwa Serikali ya Zanzibar katika kipindi chote cha maandalizi ya ufungaji wa mitambo hiyo hadi kufikia hatua ya kuikabidhi serikalini kwa ajili ya kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Sara alisema mitambo hiyo imezingatia ubora na uhitaji wa walengwa itatoa huduma kwa Zanzibar kwa kila hospitali itakayokuwa na uhitaji wa tiba hiyo.

Mitambo hiyo imegharimu zaidi ya Dola za Kimarekani 800,000 ambazo zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Global Fund ambao ni wafadhili wakuu wa mradi huo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**BERTHA RASHID BENDERA** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE255014** iliyotolewa na Idara ya uhamiaji Makao Makuu. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/225409/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**NEEMA MARIA NGIMBWA** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE480363** iliyotolewa na Idara ya uhamiaji Makao Makuu. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/225420/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MOHAMEDI MAHAMUDU ATHUMANI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba **S0958-0078** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIWANJA CHA NDEGE SEKONDARI** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/8925/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ASHRAFI TAWFIQ FRANCIS** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha sita chenye index namba **S0632/0507** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BONDENI SEKONDARI** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/220318/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KENETIA NAIBALA KILLEL** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 250 ENC** aina ya **KINGLION.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/39378/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LIMO ABDALLAH MTENGETI** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **TZQ 9952 – HONDA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/39521/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ATHUMANI OMARI SHEKIMOSHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 989 EAQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/MUH/10586/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA**

**Kituo cha MAKANG'WA Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai /Ndoa Na 64 /2024**

**Jina la Mdai DR HANCE s/o KATUNZI**

**Jina la Mdaiwa MWL. NEEMA J MALIVA**

**KATIKA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa NEEMA J MALIVA MWL SHULE YA WASIOONA BWIGIRI WILAYA CHAMWINO –DODOMA**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai)**
**MADAI YA TALAKA/KUACHANA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 24 Mwezi 10 Mwaka 2024 saa 02:30 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo..

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 16 Mwezi 10 Mwaka 2024

DODOMA

16/10/2024

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 25873 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**

**MBARAKA AZIZI MMARI……………….MAREHEMU**

**CHRISTINA JUSTINE NGUMUO……………..MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 6 Mwezi NOVEMBER, Mwaka 2024.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 17 Mwezi OKTOBA Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na…./2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ADAM SALUM MAFITA wa MJI MWEMA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA NURU ALLY MASARE**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 10 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 9 Mwezi 10 Mwaka 2024

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
CHAMWINO-MJINI
DODOMA

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 25224 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE THECLA BONIFACE LUYANGI. DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**

1. **PASCHAL WILLIAM NYAKUNGA. PETITIONER**
2. **____________________ PETITIONER**
3. **____________________ PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Under Rule 75 of Probate Rules and any other enabling Provision of the Law)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 24 day of 10.2024

Dated at MOROGORO this 16 day of 10.2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT

*PRINCIPAL/ SENIOR/ RESIDENT MAGISTRATE*
**MOROGORO DISTRICT COURT**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**INAYOKETI DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI YA GHARAMA NA. 48 YA 2022**

**CHAINA CHACHA MASWE (Msimamizi wa mirathi ya marehemu ASIA NICHOLAUS MERO)…………………………MUOMBAJI**
**DHIDI YA**

**JACKSON EZEKIELY CHARLO NA WENZAKE……MJIBU MAOMBI**

**KWA:**
**JACKSON EZEKIELY CHARLO**

**POPOTE ULIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la Maombi ya Gharama (Taxation Cause) tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es Salaam/Dodoma tarehe 1/11/2024 saa tatu kamili asubuhi (3:00).

Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hutahudhuria wewe mwenyewe binafsi binafsi au mwakilishi wako anaetambulika kisheria basi Maombi ya Gharama yatasikilizwa bila ya uwepo wako.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 17/10/2024.

D. P. KINYWAFU
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB:**

**+255 - 745 700 710.**

**E-mail:**

**advertise@guardian.co.tz,**

**website:**

**www.ippmedia.com**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe:@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Mtumba,**
**S.L.P. 2888,**
**DODOMA,**
**17/10/2024**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **18/10/2024** kampuni ya **AFRICA WAKAWAKA LOGISTICS CO. LTD** itasafirisha mzigo mkubwa kutoka Dar es Salaam kuelekea Tunduma kupitia Mikumi.

2. Gari hizo zenye namba za usajili:
   1. **T 469 EBS / T 360 EBR**
   2. **T 563 EHK / T 992 EBX**
   3. **T 285 EJG / T 764 EJE**

   VIPIMO

   **Urefu** - **22M**
   **Upana** - **4.95M,**
   **Kimo** - **5.2M**

3. Gari litasafirisha mzigo kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SANLG WORLD WIDE INVESTMENT CO. LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 202 EKR.** Chassis namba **IBRSPKB52QC302773.** Kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 205 EKR.** Chassis namba **IBRSPKB52QC302775.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/IRI/IRI/15958/2024** na **PHQ/IRI/IRI/15956/2024.**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa,Tupigie,***

**+255 - 745 700 710.**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kesi ya Gachagua yasitishwa baada ya kuumwa ghafla

**NAIROBI, Kenya**

WAKILI Mkuu Paul Muite amesema kuwa Naibu Rais wa Kenya Rigathi Gachagua amedondoka na kupelekwa hospitalini wakati wa shughuli ya mapumziko ya mchana katika kesi yake ya kuondolewa madarakani katika Bunge la Seneti.

Aidha, Naibu Jaji Mkuu, Philomena Mwilu, alisema endapo mchakato wa kumtimua Naibu Rais Gachagua utarudishwa tena mahakamani, majaji hao watafuata utaratibu ulioainishwa kwenye katiba ili kufikia hatua ya kumwondoa.

Akizungumza mbele ya Spika wa Seneti Amason Kingi, jana Muite, wakili kiongozi anayemwakilisha Gachagua, alithibitisha kuwa kiongozi huyo aliugua na kulazimika kukimbizwa hospitalini.

Muite alimwomba Spika Kingi ampe muda wa saa moja au mbili kumtembelea Gachagua na kutafakari iwapo anaweza kuendelea na kesi hiyo ama laa.

Gachagua alitarajiwa kutoa kauli yake na kuhojiwa na mawakili wanaowakilisha Bunge la Kitaifa.

"Samahani na masikitiko kwamba Naibu Rais hayupo na usumbufu na ucheleweshaji uliosababishwa kwa Spika na Seneta. Msimamo ni kwamba katika kipindi kile tulichoenda nilijaribu kujua kwanini hayupo, ukweli wa kusikitisha ni kwamba. Gachagua amechukuliwa kuwa mgonjwa na yuko hospitalini," Muite alisema.

Hata hivyo wakili mkuu anayewakilisha Bunge la Kitaifa, alitaka kesi iendelee bila Gachagua kuwepo. Na kwamba baada ya kukagua hoja zote mbili, Spika Kingi aliamuru Bunge la Seneti lisimamishwe hadi saa 5:00 usiku.

Akizungumza baada ya kikao cha seneti kusimamishwa, Seneta wa Makueni Dan Maanzo alisema kuwa Gachagua alionekana mlegevu wakati wa mapumziko ya mchana.

Seneta huyo alibainisha kuwa Gachagua anafaa kupewa nafasi ya kujitetea mbele ya Seneti kwa mujibu wa Katiba.

"Alionekana kuchoka. Kwa kweli alikula



chakula cha mchana ofisini kwake na baadhi ya Maseneta kutoka mkoa wake na wakasema yuko sawa na ghafla wakasema anaumwa ofisini kwake na kukimbizwa hospitali," Maanzo alisema.

"Kwa muda wote akiwa hospitalini, lazima apewe nafasi nzuri ya kusikilizwa kwa mujibu wa katiba na tusubiri hukumu ya spika na kama atasema tuendelee, basi hilo litakuwa na nafasi yake kisheria," alisema.

Katika hatua nyingine, Mwilu alisema utaratibu huo si wa kipekee kwa kuwa unafuata mchakato wa kikatiba na utazingatiwa kama kesi nyingine yoyote.

„Kila kitu kina kivyake kwanza hivyo kuhusu mchakato unaoendelea wa kumshtaki Naibu Rais wetu sio wa kipekee," alisema.

„Ni maombi ya katiba na sio jambo ambalo limeng'olewa hewani, lina mchakato wa kikatiba wa kufuata, inarudi mahakamani, vyovyote itakavyokuwa, ni kesi kama nyingine yoyote na itashughulikiwa kwa njia ambayo sheria imetuidhinisha kufanya," alisema.

Ilielezwa kuwa matamshi ya Mwilu yanajiri baada ya maombi 29 kuwasilishwa katika Mahakama ya Juu kusitisha mchakato unaoendelea wa kumtimua naibu huyo kuendelea hadi katika seneti.

***Citizen***

# Bil. 678/- kuleta mageuzi upakuaji mafuta bandarini

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), inatekeleza mradi wa Sh. bilioni 678.6 ambao utaboresha utaratibu wa upakuaji mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mradi huo unaohusisha ujenzi wa matangi ya mafuta ambao umefikia asilimia saba, unatarajiwa kuboresha usimamizi wa shehena ya mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam na kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kituo cha usafiri na logistiki katika Afrika Mashariki na Kati.

Akizungumza na waandishi wa habari walipotembelea eneo la mradi jana, Mhandisi wa Mradi wa TPA, Hamis Mbutu, alisema serikali iliamua kuanzisha mradi huo baada ya uchambuzi wa kina wa faida zake.

"Kwa sasa, meli ya mafuta inasubiri hadi siku 22 kabla ya kupata nafasi ya kupakua. Mradi huu utakapokamilika, muda huo utapungua hadi siku saba," alisema.

Alisema mchakato wa kupakua mafuta unatarajiwa kuanza na vifaa vilivyoko vinaweza kuwezesha meli kupakua mafuta yote kwa muda wa siku saba na baada ya kukamilika kwa mradi, muda huo utapungua hadi saa 24 pekee.

Kwa mujibu wa Mhandisi Mbutu, matangi mapya yatatoa nafasi zaidi ya uhifadhi kwa wauzaji wa mafuta ndani na nje ya Tanzania.

Alisema kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 378,000 za mafuta kwa wakati mmoja, hivyo kutoa uhifadhi wa kutosha kukidhi mahitaji ya mafuta ya Tanzania kwa muda mrefu.

Ujenzi unahusisha kujenga matangi 15 katika eneo la Kigamboni, sita kati ya hayo, yatatumika kuhifadhi dizeli, mtano yatatumika kuhifadhi petroli, matatu mafuta ya ndege na moja litakuwa la muunganisho.

"Mradi huu utaongeza kwa kiasi kikubwa uwezo wetu wa uhifadhi na kutoa fursa zaidi kwa wauzaji wa mafuta, na hivyo kuongeza vyanzo vya mapato kwa serikali," alisema Mbutu.

Kwa mujibu wa Ofisa wa Uhusiano wa TPA, Enock Bwigane, kila siku ambayo meli ya mafuta inakaa nangani kusubiri kuingia bandarini kushusha shehena ya mafuta, mtoa huduma analazimika kulipa Dola za marekani 25,000 kwa mmiliki wa meli.

"Hebu fikiria jinsi gharama zinavyoongezeka ikiwa meli itakaa kwa siku 22. Gharama hizi zote zinaelekezwa kwa mtumiaji wa mwisho kwa njia ya bei za mafuta," alisema.

Bwigane alisisitiza kuwa kupunguza muda wa kusubiri kunamaanisha bei za mafuta zitashuka katika soko la ndani pia kutakuwa na athari za kuongeza kwenye gharama zingine za uzalishaji, hivyo kuleta faida zaidi kwa watumiaji wa Tanzania.

Mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 24, ukitekelezwa na umoja wa makandarasi M/S China Railway Major Bridge Engineering Group Co.Ltd na M/S WUHUAN Engineering Co.Ltd na kupitia Liu Tao, ametoa hakikisho kwamba kazi itakamilika kwa wakati.

Mbali na ujenzi wa matangi, awamu ya kwanza itajumuisha usakinishaji wa pampu, vifaa vya kupimia, mifumo ya kinga ya moto, na mita za mtiririko. Pia kutajengwa bomba la mafuta lenye urefu wa kilomita 5.5 kuunganisha mifereji ya TPA kati ya Kigamboni na Kurasini.

Tao alisema hatua ya kuhamasisha inakaribia kukamilika, huku Ripoti ya Tathmini ya Athari za Kijamii na Kimazingira ikiwa tayari kwa ajili ya kuwasilishwa kwa Baraza la Usimamizi wa Mazingira la Taifa (NEMC)

Pia alisema maandalizi ya eneo ikiwamo kuondoa vifusi, yamefanyika kwa ufanisi kwa kutumia magari 20 ya kuondoa taka, excavator tatu, na buldoza mmoja.

"Tunaendelea kusukuma kwa nguvu kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na uzinduzi wake ufanyike Agosti 2026," alisema Tao.

Mkataba wa usanifu na ujenzi wa matangi ya kuhifadhi na kusambaza mafuta ulitiwa saini Februari, mwaka huu, huku eneo likikabidhiwa rasmi kwa mkandarasi Agosti 16.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, hivi karibuni alieleza mipango zaidi ya kuongeza uwezo wa bandari, ikiwamo ujenzi wa gati mpya kuanzia gati namba 12, 13, 14, na 15 katika Bandari ya Dar es Salaam ili kuboresha uwezo wa kushughulikia mizigo.

## Walipakodi wakubwa TRA watengewa ofisi maalum

**Na Grace Gurisha**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imefungua ofisi maalum kwa ajili ya walipakodi binafsi wenye hadhi ya juu, ili kuwaaangalia kwa ukaribu na walipe kile wanachostahili kuepuka matatizo baada ya kufanyiwa ukaguzi.

Walipakodi hao ni wamiliki wa kampuni wanaoingiza Sh. bilioni 20 kwa mwaka, wamiliki wa hisa wanaoingiza zaidi ya Sh. bilioni 2.5, viongozi wanaomiliki kampuni na wale wenye ubia kwenye kampuni wanaoingiza Sh. bilioni 20 kwa mwaka.

Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda, alisema hayo jana wakati akifungua ofisi hiyo jijini Dar es Salaam huku akisisitiza kuwa alisema lengo ni kuendelea kuimarisha huduma za kikodi kwa walipakodi.

Alisema wameanza na walipakodi 158 ambao mapato yao ni makubwa, wanamiliki kampuni, wameajiri watu na kampuni zao zinalipa kodi na wao wanapaswa kulipa kodi kama waajiriwa wengine.

"Tumeanza na hawa 158, walipakodi binafsi wako 111 wote wameshaitwa hapa na viongozi wa mihimili mitatu ya juu wako 47. Tunawapa huduma bora kwa sababu wana mchango mkubwa. Tukiwaacha wakakosea kidogo, tutakosa mapato," alisema.

Kamishna mkuu huyo alisema lengo ni kuangalia kodi zao na si kampuni zao, hivyo hiyo wanahitaji kupata elimu ya kutosha mara kwa mara na pia wanahitaji kuangalia kile wanachostahili walipe.

"Hii ni uthibitisho kwamba hawa nao wanalipa kodi kama wengine. Kama mwajiriwa anavyolipa na hawa pia walipe. Kanuni yetu ya mfumo nzuri wa kodi inawataka wenye uwezo mkubwa kama hawa walipe kodi inayotakiwa.

Pia alisema kuna kundi lingine la viongozi wataenda baadaye katika ofisi hiyo, ambapo watakuwa wanahudumiwa hapo kutokana na mapato ya shughuli wanazofanya kama ajira na wao wataangaliwa kwa ukaribu na kushauriwa ili wachangie kile wanachostahili.

"Hawa wanatakiwa kuchangia asilimia 30 ya mapato yao kama anachokipata kwenye shughuli zake, wanakuwa na shughuli nyingi wanaweza wakawa na kampuni, wanaweza wakawa wamewekeza au wakawa na biashara zingine. Kwa hiyo mapato yale yote, sasa hivi yatakuwa yanaangaliwa kwa pamoja," alisema.

# Bank of India (Tanzania) Ltd.

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

*Relationships beyond banking*

## DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019

### MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

**Service Charges (Exclusive of VAT and Government Levy on DigitalTransactions) (The applicable VAT (Value added Tax) and Govt Levy on digital Transaction to be collected during the collection of service charges)**

### A. REMITTANCE –OUTWARD

| Sr. No. | Item | Charge in TZS or Equivalent to TZS |
|---|---|---|
| **TISS Remittance** (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | Remittance -TZS or TZS Equivalent Transaction value | |
| | Between TZS 1 to 10 million | 2,000 |
| | Between TZS 10 million to 50 million | 5,000 |
| | Above TZS 50 million | 10,000 |
| | | |
| **TIPS AND TACH** | Transaction value | |
| | Between TZS 1-TZS 50,000 | 500 |
| | Between TZS 50,001-TZS 500,000 | 1,000 |
| | Between. TZS 500,001- 5,000,000 | 1,500 |
| | Between. TZS 5,000,001- 20,000,000 | 2,500 |
| | | |
| **Other Outward Remittance** | 1USD up to 6,000 | USD 15 |
| | USD 6,001 – 10,000 | USD 30 |
| | Above USD10,000 | @ 0.35% Maximum USD 75 |
| Tracer Charges | Irrespective of Amount | USD 30 |
| Recall back funds charges | Irrespective of Amount | USD 30 |

### B. REMITTANCE –INWARD

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | From inside Tanzania (TISS, TIPS AND TACH) | Free |
| | From outside Tanzania: as under | |
| | For Current /Overdraft Accounts | 0.35% of inwards remittance Minimum USD 18 Maximum USD 70. |
| | For Saving Accounts | |
| | USD 0 up to USD 100 | Free |
| | USD 101 up to USD 500 | USD 10 |
| | Above USD 500 | USD 18 |

### C. DEPOSIT AND RELATED SERVICES

| Item | TZS A/c | USD A/c |
|---|---|---|
| **Saving Account :-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 2000 |
| Cash withdrawal charges over USD 2,000 to USD 5000 per day | -- | 0.25% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25 Mn per day | 0.10% of withdrawal amount | |
| Cash Deposit charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of deposited amount |
| Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both for below and above USD 5,000) | -- | 12% (Min USD 1) of the aggregate small currency amount |
| **Current Account:-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 5000 |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdrawal amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | 0.15% of withdrawal amount | -- |
| Cash deposit charges over USD 10,000 per day | | 0.60% of deposit |
| **Maintenance of minimum balance: -** | | |
| For Saving Account-Without Cheque Book Facility | TZS 50,000 | USD 50 |
| With Cheque Book Facility | TZS 200,000 | USD 200 |
| For Current Account | TZS 200,000 | USD 200 |
| **Minimum balance charges (in case of non-maintenance of minimum balance)** | | |
| Saving Account - Without cheque book | TZS 900 p.m | USD 4 p.m |
| With cheque book | TZS 3600 pm | USD 15 p.m |
| Current Account- | TZS 20,000 p.m | USD 15 p.m |

### D. Other Common Charges

| Item | Charges | |
|---|---|---|
| | TZS A/c | USD A/c |
| Stop Payment Instructions | TZS 35,000 | USD 28 |
| Regular statement of a/c (Monthly) | Free | Free |
| Interim/additional statement | TZS 1500 per page | USD 1.50 per page |
| Issue of bankers' cheque | TZS 40,000 | USD 30 |
| Cancellation of bankers cheque/DD | TZS 20,000 | USD 15 |
| Issue of Duplicate Bankers cheque/Demand Draft/ Duplicate FDR | TZS 30,000 | USD 20 |
| Application charge for Treasury Bond | TZS 100,000 | USD Equivalent to TZS 100,000 |
| Issue of Balance certificate (Saving Account) | TZS 20,000 | USD Equivalent to TZS 20,000 |
| Issue of Balance certificate (Current Account) | TZS 50,000 | USD Equivalent to TZS 50,000 |
| Signature verification and Photo Attestation charges for Domestic A/c Holders | TZS 10,000 | USD Equivalent to TZS 10,000 |
| Verification of Documents such as KYC Documents along with verification of Photo and Signature of Customer Mentioned account with Bank of India- in India /Overseas | TZS 25,000 | USD Equivalent to TZS 25,000 |
| Savings bank customer Identification card-One time | TZS 20,000 | USD 10 |
| Dormant a/c Activation Per Activation Fees | Individual TZS 5,000 Corporate TZS 12,000 | Individual USD 3 Corporate USD 6 |
| Account Freezing/un freezing Charges | Free | Free |
| SMS Alert facility | Free | Free |
| Email Alert Facility | Free | Free |
| Monthly Statement on Registered Email | Free | Free |
| Balance Inquiry (Over the Counter) | Free | Free |
| Charges for Deletion of Decease Person Name from the Saving Account | Free | Free |
| Charges for Addition/modification Account such as Change in respect of Corporate A/c | TZS 20,000 | USD 10 |
| Updating of Mobile No. in A/c (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Change /Modification in Address (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Issuance of No Dues Certificate for Non-Borrowers. | TZS 10,000 | USD 7 |
| Ledger Folio Charges per Folio (40 lines per Folio) only for Current and Overdraft Accounts | TZS 6,000 per Folio | USD 4 per Folio |
| Postages/Courier Charges Inland/Foreign | TZS 30,000 or actual charges whichever is higher | USD Equivalent to TZS 30,000 |

### E. CLEARING SERVICES

| Item | Charge/Fees | |
|---|---|---|
| | TZS A/c | USD A/c |
| Within walking distance-1 km | TZS 70,000 | USD 45 |
| Far off distance –more than 1 km | TZS 95,000 | USD 65 |
| Cheque returned charges –financial reasons (inward/outward) | TZS 70,000 | USD 55 |
| Inward/outward cheque collection - USD | 0.60% Min comm.18 postages 90 | 0.60% Min comm.18 postages 90 |

### CREDIT MATTERS

| Charge/Fees | |
|---|---|
| | |
| **Proposal Processing Charges: -** | |
| New Overdraft/Term Loan/Demand Loan | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| TOD/TOL/ADHOC | Proportionate to 1.50% for TOL/TOD/ADHOC Period minimum USD 60 |
| New NFB BG/LC Facility | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| Review of Overdraft Limit | 1.50% on entire sanctioned amount. |
| Review of Term Loan Demand Loan Personal Loan Vehicle Loan Loan Against Property Etc. | 0.15% maximum USD 600 or TZS 1.20Mn on the reviewed amount and 1.50% on the additional Term Loan /Demand Loan amount. |
| Schematic Lending up to 36 months/Staff Loan | Nil |
| Prepayment charges | 2.50% of the prepaid loan amount. |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges |
| | 1) No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered. 2) Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit |
| | **We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -** 1) Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee 2) Release of Personal Guarantee/Collateral Security. 3) Interchangeability of limits. 4) Change in project/items of Machinery 5) Ceding of charges on assets(Pari-Passu) 6) Restructuring, Rephasement of Loans/ Deferment of Loan installments. 7) Approvals for mergers & amalgamations. 8) Any other miscellaneous credit related approvals. |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where** **We are Lead bank: Nil** **We are Not Lead Bank:** USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free **USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** |
| Non/Delayed Submission of Audited Financial Statements of the Company OR wherever applicable | **USD 100 or equivalent in TZS per month or part thereof** |
| | **Note:-**Audited Financial statements of the firm/company within 6 months from closure of Financial Year or as approved by TRA for the relevant year. |
| Inspection charge | **TZS 50,000** or equivalent to USD per visit /inspection or at least once in quarter whichever is higher. |
| | **Note:-** 1) Out of Pocket Expenses to be recovered additionally along with regular inspection charges wherever applicable 2) **Project Monitoring Inspection Charges/Technical Due Diligence Inspection charges:** Considering the fact that this inspection is proposed for safeguarding banks Interest, normal inspection charges besides travelling, boarding/lodging expenses are to be recovered from the borrower. |
| Issuance of No objection certificate (NOC) | **USD 100 or equivalent in TZS** |
| 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) | Waiver of Processing & Documentation charge. |
| Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) | For Overdraft account 0.50% of Sanction Limit. For Term Loan/Demand Loan 0.50% of O/s Amount |
| Earmarking of Limits | **USD 500 or equivalent in TZS per annum** |
| Non Compliance of Sanction terms/Commitment charges | **1.00% additional Penal Interest to be charge till compliance of Sanction terms** |

| **D&B/ Other Credit Information Search for per Borrowal a/c (New/Additional/Review of limit)** | | |
|---|---|---|
| Up to TZS 20 Mn/USD 10,000 (Only for new and additional Limit. **Review – No charge**) | USD Facility | TZS Facility |
| | USD 5 | TZS 5,000 |
| Over USD 10,000 to USD 50,000/ Over TZS 20 Mn up to TZS 100 Mn | USD 10 | TZS 20,000 |
| Over USD 50,000/TZS 100 Mn | USD 50 | TZS 100,000 |
| D&B Search for non-Borrower, on request | USD 50 | TZS 100,000 |
| Charges for Furnishing copy of Credit Information report obtained from CIC | **TZS 20,000** | **USD 10** |

| **Guarantee (Performance/Financial) :-** | |
|---|---|
| Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part thereof minimum for one quarter. |
| Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate |
| Swift Charges | **As Applicable** |
| Postages | **As Applicable** |
| Revert of Guarantee before Expiry | **Minimum 1 Qtr BG Commission to be recovered for part of quantum of full guarantee commission to be recovered** |
| Closure of Guarantee After Expiry of Claim Period | Nil |
| Invoke of Guarantee | **USD 200 or equivalent in TZS** |
| | **A. Financial Guarantees: -** 1. In favour of Customs/Excise/Tax Authorities towards tax/Duties payment Etc. 2. Favouring Courts for Release of Amounts. 3. For Guaranteeing Loan payments. **B. Performance Guarantees: -** 1. In lieu of earnest money deposit 2. In lieu of tender deposit 3. In lieu of security deposit 4. To obtain advance payments (generally exports) 5. To obtain mobilization advance (generally domestic) 6. Towards Direct/indirect taxes to govt. in respect of specific transaction. 7. For Direct/indirect taxes disputes with tax Authorities. 8. For payment for supplies/services made /rendered 9. For Securing retention amount 10. For Bidding/tendering for Project Contacts 11. For Performance in terms of any agreed contact. **Note: - No processing charges or documentation charges are to be levied in case of Casual BG limits issued against 100% or more cash margin.** |
| **Imports :-** | |
| LC Opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| Against 100% cash margin | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| LC Amendment Charges | Per amendment 0.40% of LC amount (minimum USD 60 and Maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (Same for LC against 100% cash margin) |
| Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 180 |
| Retirement of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 360 |
| Inward Bills for Collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 |
| **Exports:-** | |
| Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount Minimum USD30 Maximum USD 360 |
| Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30/- |
| LC Advising Charges | USD 150 |
| Export Bills for Collection | 0.60% of Bill amount Minimum USD 30 Max USD 360. |
| Charges for Certifying invoices subsequent to negotiation | **USD 10 Per Invoice** |
| Clean payment Received under LC | **USD 100 per occasion** |
| Advice of transfer in transferable LC | **USD 100 per advice of transfer and acceptance commission at 0.30% Minimum USD 100** |

### OTHER DISCLOSURES
### (VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Base or Prime Lending rate** | 7.50% p.a. | 14.50% p.a. |
| **2.0** | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| **3.0** | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| **4.0** | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | **Up to USD 10,000** | **Up to TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.00% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.50% | 7.25% |
| | | **Over USD 10,000** | **Over TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.50% | 6.75% |
| | Over 6 months | 4.00% | 7.75% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |
| | | | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashish Kumar Jha | Managing Director | Signed | 10.10.2024 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 10.10.2024 |
| 3. | Robert Kibona | General Manager | Signed | 10.10.2024 |

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### REAL WAMKOMALIA ALEXANDER

REAL Madrid wameufanya usajili wa mlinzi wa Liverpool na England, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26 kuwa kipaumbele. ***(Athletic)***

### NICOLO BARELLA AITAJIKA ENGLAND

LIVERPOOL na Manchester City wanavutiwa na Nicolo Barella wa Inter Milan mwenye miaka 27, lakini kiungo huyo wa kati wa Italia yuko kwenye rada za Real Madrid na Atletico Madrid. ***(Fichajes)***

### ARSENAL YAMNYATIA SESKO

ARSENAL inafuatilia maendeleo ya mshambuliaji wa Red Bull Salzburg na Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 21, huku wakianza kujipanga kwa ajili ya usajili wa dirisha lijalo. ***(Football London)***

### CRYSTAL YAWEKA NGUMU KWA SARR

KLABU ya Crystal Palace haiko tayari kukaribisha ofa zozote kwa mshambuliaji wa Senegal, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 26 Januari. ***(Football Insider)***

### MONTELLA ATAJWA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United imemwongeza kocha wa Uturuki na mshambuliaji wa zamani wa Italia, Vincenzo Montella mwenye miaka 50, kwenye orodha yao ya watu wanaotarajiwa kuchukua nafasi ya kocha wao wa sasa, Erik ten Hag mwenye miaka 54, Old Trafford. ***(Ajansspor)***

### ERIKSEN ATAFUTIWA MRITHI UNITED

KLABU ya Manchester United inapanga kusajili viungo watakaochukua nafasi ya Christian Eriksen mwenye miaka 32, pamoja na Casemiro mwenye miaka 32. ***(Football Insider)***

### MAN UNITED WAMTAKA DE JONG

MANCHESTER United pia iko tayari kumsajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 27, ikiwa ataondoka Barcelona msimu ujao. ***(Fichajes)***

### ACHERAMPONG ATAKIWA MADRID

REAL Madrid inafikiria kumnunua mchezaji wa kimataifa wa England, Josh Acheampong ifikapo Januari huku Liverpool, Newcastle United na Tottenham Hotspur pia wakimtaka beki huyo wa kulia wa Chelsea**.** ***(Independence)***

### MOYES KUTUA CRYSTAL PALACE

KLABU ya Crystal Palace inamtaka, David Moyes mwenye umri wa miaka 61, kuchukua nafasi ya kocha, Oliver Glasner mwenye wa miaka 50, baada ya kuanza vibaya msimu wa Ligi Kuu ya England. ***(Caughtoffside)***

### GUÉHI ATAKIWA NEWCASTLE

UTEUZI wa Thomas Tuchel kama kocha wa England umeongeza matumaini ya Newcastle United ya kumsajili mlinzi wa Crystal Palace, Marc Guehi mwenye miaka 24, huku Eddie Howe sasa akiwa na uwezekano mkubwa wa kusalia St James' Park. ***(Givemesport)***

### BADE ANYATIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL ipo kwenye mazungumzo na Sevilla kuhusu kumnunua mlinzi wa Ufaransa, Loic Bade mwenye miaka 24. ***(Todo Fichajes)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# THOMAS TUCHEL AANIKA MIKAKATI YAKE ENGLAND

## ●●●Ajipanga kuifanya timu hiyo kushinda na kusahau yaliyopita...

**LONDON, England**

KOCHA mpya wa England, Thomas Tuchel amefichua nia yake ya kuunda aina ya uchezaji na utamaduni wa kushinda ambao utasahaulisha yaliyopita atakapoanza kazi Januari.

Tuchel ameteuliwa kuwa mrithi wa kudumu wa Gareth Southgate kwa mkataba wa awali wa miezi 18 hadi mwisho wa Kombe la Dunia la 2026, akiwa na jukumu la kukabidhi kombe la kwanza la wakubwa la kimataifa katika soka la wanaume tangu walipofanya hivyo miaka 60 iliyopita. England ilifika fainali za Ubingwa wa Ulaya chini ya Southgate mwaka 2021 na 2024, ikikosa ubingwa katika vipindi vyote hivyo.

Kinyume chake timu ya Taifa ya Wanawake ilishinda ubingwa wa Ulaya mwaka 2022 na pia kufika fainali ya Kombe la Dunia mwaka mmoja baadaye, wakati mataji ya Kombe la Dunia la Wanaume chini ya miaka 17 na 20 yalipatikana 2017, pamoja na taji la Ulaya la chini ya miaka 21 lilipatikana mwaka jana pia.

Alipoulizwa na BBC Sport ikiwa anaamini madai kwamba kuwa kocha mkuu wa wanaume wa England ni ngumu kwake, Tuchel alitoa mpango wake wa kuvunja mzunguko wa kutofaulu.

"Hakuna lisilowezekana katika michezo," alisema.

"FA ipo, wanawake walifanya hivyo, vijana wa chini ya miaka 21 walifanya hivyo, kwa hiyo hakuna sababu ya kushindwa. Nadhani wakati fulani lazima tujikomboe kutoka kwenye historia. Tunapaswa kuzingatia juu ya mchakato na hii itaanza Januari.

"Halafu, tunahitaji kutafuta miongozo, tunahitaji na kanuni, labda pia kutoka kwa soka la klabu ambayo mimi, wafanyakazi na wachezaji tunaweza kuishi kulingana na wakati pale tunapohitajika kufanya hivyo.

"Kutoka hapo, natumaini kuunda mtindo wa kucheza, lakini pia mazingira ambayo yanatusukuma kwa asilimia ya ziada ambayo inahitajika. Kisha, bila shaka, tunahitaji bahati kidogo, tunahitaji kufuzu kwa Kombe la Dunia, tunaamini tunaweza kufanya hivyo."

Southgate alikuwa bosi wa timu ya wanaume aliyefanikiwa zaidi England, lakini bado alizomewa katika Euro 2024, ingawa timu yake ilifika fainali.

# Messi: Martínez anastahili Ballon d'Or 2024

**BUENOS AIRES, Argentina**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Argentina na mshindi mara nane wa Ballon d'Or, Lionel Messi amesema anaamini mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez anastahili kutwaa tuzo ya Balon D'or ya 2024.

Baada ya mchezo wa Jumanne usiku ambao Argentina iliitandika Bolivia mabao 6-0, Messi na Lautaro Martinez wote wakiingia kambani, alisema mshambuliaji huyo mwenzake anastahili tuzo hiyo.

Messi alisema umekuwa msimu mzuri kwa Martinez ambaye ameshinda Copa America na timu yake ya taifa, taji la Serie A akiwa na Inter pamoja na kuchukua kiatu cha dhahabu cha Copa America akiwa na mabao matano hivyo haoni sababu ya mshambuliaji huyo kukosa Ballon d'Or.

„Amekuwa na mwaka mzuri sana, alifunga katika mechi ya fainali, alikuwa mfungaji bora Copa America, nadhani anastahili Ballon d'Or kuliko mtu yeyote," alisema Messi.

Martinez ni mmoja wa nyota waliosalia katika orodha inayojumuisha nyota 30 wanaowania tuzo hiyo ambayo itatolewa usiku wa Oktoba 28 jijini Paris nchini Ufaransa na mshindi huyo mara nane wa tuzo hiyo anaamini Lautaro ni mtu sahihi.

Tuzo hiyo yenye heshima kubwa duniani itakuwa na mmiliki mpya mwaka huu huku majina ya nyota wanaosumbua kwa sasa ulimwenguni ni Erling Haaland, Phil Foden, Ruben Diaz na Rodri wa Manchester City, Jude Bellingham, Vinicius Jr na Kylian Mbappé wa Real Madrid, Martinez pamoja na Bukayo Saka na Martin Odegaard kutoka Arsenal.

# Majeruhi Man Utd yamuumiza Ten Hag

**MANCHESTER, England**

KOCHA Mkuu wa Manchester United, Erik ten Hag, atakutana na ugumu wa kupata kikosi cha kwanza pindi Ligi Kuu ya England itakaporejea kutokana na wingi wa majeruhi ndani ya kikosi chake.

Duru zinaeleza kuwa Luke shaw na Tyrell Malacia wameonesha maendeleo makubwa kwenye majeraha yao, lakini hawatarajiwi kuwa imara vya kutosha kuwavaa Brentford wikiendi hii ikimwongeza msongo wa mawazo Ten Hag ambaye amekuwa akihangaika na ufiti wa wawili hao tangu kuanza kwa msimu huu.

Beki wa kushoto, Diogo Dalot na wa kulia Noussair Mazraoui wamekuwa nguzo ya United msimu huu, bahati mbaya Mazraoui anatarajiwa kukosa wiki kadhaa baada ya kufanyiwa upasuaji mdogo wa moyo na kumwacha Dalot kuwa chaguo la pekee kwa Ten Hag.


Mashabiki wa Man United kwenye mitandao ya kijamii wamekuwa wakililia kupewa nafasi kwa kinda mwenye umri wa miaka 17 wa akademi ya klabu hiyo, Harry Amass.

Hata hivyo Ten Hag amekuwa akisisitiza kuwa kijana huyo hajakua kubeba majukumu ya timu ya wakubwa.

Man United wanashika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England wakishinda mechi 2, sare 2 na vipigo 3.

Wamefunga mabao 8 na kufungwa 10 baada ya mechi saba walizocheza na kesho Jumamosi watawakaribisha Brentford dimbani Old Traffor.





# POGBA: NILIFIKIRIA KUSTAAFU SOKA BAADA YA KUFUNGIWA

**PARIS, Ufaransa**

PAUL Pogba amefichua kuwa alifikiria kustaafu baada ya awali kufungiwa kuchezea soka kwa miaka minne kwa matumizi ya dawa za kusisimua misuli.

Pogba mwenye umri wa miaka 31 sasa amepunguziwa adhabu yake hadi miezi 18 na Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo (CAS) baada ya kukata rufani, hiyo ikimaanisha kuwa anaweza kurejea kwenye soka la kulipwa Machi 2025.

Alipoulizwa na ESPN kama alifikiri angewahi kucheza tena baada ya uamuzi wa kwanza Februari, Pogba alisema: „Ndio, nilikuwa na mawazo mengi kichwani mwangu, nilikuwa na mawazo mengi hata kuacha kucheza.

"Nilifikiria, ‚Nitafanya nini?' Ikiwa ni miaka minne, unaanza kufanya hesabu kichwani mwako, miaka minne sijacheza, nikifanya mazoezi ni klabu gani itanitaka na mambo kama hayo, unatengeneza picha nyingi kwenye kichwa chako.

"Lakini kwa upande mwingine, nilikuwa na imani dhahiri, na nilikuwa na uhakika. Nilijua sikufanya chochote kibaya kwa makusudi, kwa hiyo kwa shukrani hiyo ilitokea na walipunguza."

Kiungo huyo wa kati wa Ufaransa alipatikana na hatia ya kututumia dawa za kusisimua misuli zilizopigwa marufuku Agosti 2023 baada ya mechi ya ufunguzi ya Juventus ya msimu wa 2023-24 dhidi ya Udinese.

Mechi yake ya mwisho ya kulipwa ilikuja dhidi ya Empoli Septemba 3, 2023, kabla ya habari za matokeo mabaya ya vipimo vyake kuibuka.

Pogba aliongeza kuwa sakata hilo limemfanya awe na hekima zaidi kama binadamu.

"Unapokaa na kuona jinsi mambo yalivyopitia maisha yangu yote, sio dawa za kuongeza nguvu tu, mimi nadhani ni kama nilipata miaka 10 zaidi, nilipata uzoefu zaidi, busara zaidi," alisema.

„Na ilinifanya kutambua wakati mwingine unapaswa kuwa mwangalifu zaidi kwa uamuzi unaochukua."

# SINGIDA YAWAPELEKA YANGA, COASTAL UNION NEW AMAAN

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Singida Black Stars imetangaza rasmi mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya mabingwa watetezi, Yanga itachezwa Oktoba 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

Sababu kuu ya kuupeleka mchezo huo Zanzibar ni mabadiliko yaliyofanywa na Bodi ya Ligi Kuu lakini pia kupisha ukarabati wa Uwanja wa Liti.

Ofisa Habari wa Singida Black Stars, Hussein Massanza, alisema sababu hizo mbili zimepelekea mabosi wa klabu hiyo kufanya uamuzi huo.

"Mnakumbuka Bodi ya Ligi imetangaza mabadiliko ya ratiba, mchezo wetu dhidi ya Yanga awali hakukuwa umepangiwa tarehe ingawa ulikuwapo kwenye ratiba, kwa sasa umepangwa kuchezwa Oktoba 30, mechi yetu dhidi ya Azam, iliyopaswa tucheze Novemba 3, imerudishwa hadi tarehe 27, mwezi huo.

Vile vile mchezo wetu dhidi ya Coastal Union ambao katika ratiba ya awali ulikuwa uchezwe Novemba 7, mwaka huu umerudishwa nyuma hadi Novemba 2, tuna michezo mingine ya nyumbani dhidi ya Namungo na Fountain Gate, sasa kuna mabadiliko ya viwanja kwa sababu zote hizo hatutacheza kwenye uwanja wetu wa nyumbani," alisema Massanza.

Aliongeza tayari Bodi ya Ligi imetangaza kutoridhishwa na baadhi ya hali ya viwanja, hivyo michezo yao miwili dhidi ya Yanga na Coastal Union wataicheza kwenye Uwanja wa New Amaan ili kutoa muda wa kuukarabati uwanja wao wa Liti.

"Sisi tuna uzoefu, ukishaanza kuona hivyo ujue kuna dalili za kufungiwa uwanja, halafu tutaanza kutangatanga kutafuta viwanja vingine, kutokana na hilo tulikaa kama uongozi wa klabu katika vikao vya ndani, akiwamo meneja wa uwanja, akatuambia mechi nne zote zisichezwe kwenye uwanja huu utafungiwa," Massanza alisema.

Kutokana na tahadhari hiyo, mechi mbili tu kati ya nne watacheza kwenye uwanja huo, ambapo itacheza dhidi ya Namungo na Fountain Gate huku ile ya Yanga na Coastal Union wataipeleka kwenye Uwanja wa Amaan.



Straika wa Ngorongoro Heroes, Shekhan Khamis (kulia), akiwania mpira dhidi ya nyota wa timu hiyo wakati wa mazoezi ya kujiandaa kuivaa Uganda katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya CECAFA U-20 itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Ngorongoro mechi muhimu CAF

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), inatarajia kuwakaribisha Uganda katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-20), itakayochezwa leo kuanzia saa 9:00 mchana kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Mechi nyingine ya hatua hiyo inatarajiwa kuwakutanisha Kenya dhidi ya Burundi, itachezwa muda kama huo kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Timu mbili zitakazofanya vyema zitapata tiketi ya kuiwakilisha CECAFA katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-20), zitakazofanyika baadaye mwakani.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Ngorongoro Heroes, Boniface Mkwasa, alisema wachezaji wake wameimarika na wamekuwa wakionyesha kiwango kizuri kadri mashindano hayo yanavyoendelea.

Mkwasa alisema anaamini watapata matokeo mazuri katika mechi hiyo na malengo yao makubwa ni kubeba ubingwa wa michuano hiyo mwaka huu.

"Mimi ni mzoefu na mashindano haya, timu inaweza kuanza vibaya, lakini uko mbele ikabadilika na hiki ndio kinaonekana, nawapongeza vijana kwa kuendelea kupambana. Kwetu kila mchezo ni muhimu na wao wanazidi kuzoea mashindano," alisema Mkwasa.

Aliongeza anafahamu Uganda wana kikosi kizuri na wataingia uwanjani kwa kuwaheshimu.

"Uganda ni moja kati ya timu yenye wachezaji wazuri, wenye nguvu na vipaji vya kucheza soka, tuko tayari kwa mchezo huu, tunawaheshimu Uganda, lakini lengo letu lazima litimie, tukishinda kesho (leo), tutakuwa tumefuzu AFCON, lakini bado tunahitaji pia ubingwa wa CECAFA," alisema kocha huyo.

## Simba: Mashabiki wetu wanatudai

INATOKA UK. 24

mechi ya mwisho kabla ya kwenda kwenye majukumu ya kimataifa," aliongeza beki huyo wa pembeni wa Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Naye Shomari Kapombe, ambaye ni mchezaji mwandamizi wa timu hiyo iliyoko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi alisema wachezaji wote wapo tayari kwa ajili ya kusaka ushindi kwenye mchezo huo wa kesho.

Beki huyo wa zamani wa Azam FC amewataka mashabiki na wanachama wa Simba kutokuwa na wasiwasi kwa sababu wamejipanga kuwalipa furaha.

"Benchi letu la ufundi linaendelea kufanya kazi yake na sisi wachezaji kazi yetu itaonekana uwanjani Jumamosi (kesho), naamini tutafanya vizuri, tunajua namna mashabiki wetu wanavyoisubiria hiyo mechi, huu ni msimu wao," Kapombe alisema.

Ubora na ushindani uliopo kwa wachezaji wa timu zote mbili unaufanya mchezo huo wa dabi kusubiriwa kwa hamu na idadi kubwa ya mashabiki kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Singida Black Stars yenye pointi 16 kibindoni, ikiwa imeshinda mitano na sare moja, ikifunga magoli tisa na kuruhusu nyavu zake kuguswa mara tatu, ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Simba yenye pointi 13, imecheza mechi tano.

Yanga ina pointi 12 na imeshuka dimbani mara nne tu, iko katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali.

Vigogo hao wawili wote wametinga hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa, Yanga ikipanga Kundi A kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Wekundu wa Msimbazi pia wakiwa Kundi A kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

## Bacca ashusha presha Yanga

INATOKA UK. 24

lekea mechi hiyo na hawana maneno zaidi ya kuzungumza kwa sababu wanasubiri muda wa vitendo.

"Tupo kambini kwa ajili ya mechi hiyo itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kila kitu kinaenda vizuri, kila mtu anajua nini anatakiwa kukifanya, nadhani nilishazungumza hapo awali, aina hii ya michezo si ile ambayo benchi la ufundi wanalazimika kuongea sana kwa sababu inajizungumza yenyewe kwa ukubwa wake," aliongeza kiongozi huyo.

Taarifa hiyo ya Harrison, imeleta faraja kwa wanachama na mashabiki wa Yanga, ambao waliingiwa na wasiwasi ya kumkosa beki huyo ambaye amekuwa tegemeo kubwa katika eneo la ulinzi.

Kwa upande wa Simba, mashabiki wao walishaanza 'kuwakoga' wenzao wakitamba endapo beki huyo atakosekana, timu yao inajiandaa kupata idadi kubwa ya mabao kutokana na hali ya mastraika wao wanaoongozwa na Leonel Ateba.

# Michezo

Ijumaa Oktoba 18, 2024

Nipashe



**Majeruhi United yamuumiza Ten Hag** UKURASA 22




# Simba SC: Mashabiki wanatudai

## Ni maneno ya wachezaji, waahidi ushindi ili kuwafuta majonzi...

**Na Faustine Feliciane**

IKIWA imebaki siku moja kabla ya mchezo wa Dabi ya Kariakoo, baadhi ya wachezaji waandamizi wa Simba wamesema wanaona wanadeni kwa mashabiki wao hivyo lazima wapambane na kuhakikisha wanapata ushindi dhidi ya Yanga hapo kesho.

Simba atakuwa mwenyeji katika mchezo huo wa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa mwaka 2024/2025.

Yanga ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi wa mechi zote mbili za msimu uliopita, lakini pia ikiwafunga Simba bao 1-0 kwenye mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, nahodha wa Simba, Mohamed Hussein ‚Zimbwe Jr' alisema wanafahamu umuhimu wa mchezo huo na mategemeo ya mashabiki wao.


Zimbwe alisema kwao wanaichukulia mechi hiyo ina umuhimu mkubwa ‚sana' hasa baada ya kutofanya vizuri katika michezo mingine ya dabi waliyocheza hivi karibuni.

"Tunaendelea na maandalizi yetu vizuri, tunaahidi tutapambana ili kuhakikisha tunawalipa mashabiki wetu, upendo na hamasa yao wanayotupa sisi kwetu kama wachezaji ni sawa na deni," beki huyo wa zamani wa Kagera Sugar alisema.

Aliongeza matokeo ya mwisho ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union hayakuwa mazuri na kwao wanayachukua kama funzo kuelekea katika mchezo dhidi ya watani zao.

"Mashabiki waendelee kutusapoti, tutapambana kwa kila namna kuhakikisha tunapata ushindi, tunajua tuliwaumiza katika


INAENDELEA UK. 23

Bacca

# Bacca ashusha presha Yanga

**Na Adam Fungamwango**

HALI ya beki wa kati wa Yanga, Ibrahim Abdallah ‚Bacca' ni nzuri na mlinzi huyo atacheza mechi dhidi ya watani zao, Simba itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, imeelezwa.

Yanga imelazimika kutoa kauli hiyo kufuatia tetesi huenda Bacca akaukosa mchezo huo kwa sababu ni majeruhi.

Sintofahamu hiyo imeenea baada ya beki huyo kuweka picha ya kupata jeraha kwenye kifundo chake cha mguu baada ya kumalizika kwa mechi kati ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), dhidi ya DR Congo, iliyochezwa Jumanne hapa nchini.

Hata hivyo Bacca hakuandika maneno yoyote katika picha hiyo, ingawa baadhi ya wachambuzi walidai Mzanzibar huyo aliumia katika mechi hiyo ambayo Stars ililala mabao 2-0.

Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema jana mchezaji pekee ambaye ni majeruhi katika kikosi chao ni Farid Mussa lakini ameshaanza mazoezi maalum ya kurejesha utimamu wa mwili, kabla ya kujumuika pamoja na wenzake.

"Hakuna taarifa yoyote ya majeruhi, na wachezaji wote waliokuwa kwenye vikosi vya timu za taifa, wameshawasili, hakuna yoyote aliyerejea akiwa na majeraha, mtu pekee ambaye bado na matatizo ni Farid, na yeye pia ameshaanza mazoezi mepesi ili kurudisha utimamu wa mwili kabla ya kujiunga na wenzake.

Nasema hakuna taarifa yoyote nyingine ya upande wa majeraha ya wachezaji wetu, kikosi chetu kiko imara na tayari kwa dabi hiyo," Harrison alisema.

Kuhusu mchezo husika, meneja huyo alisema maandalizi yao yanaendelea vizuri kwa sababu walikigawa kikosi chao pande mbili.

"Kila kitu kinaenda vizuri, tumekuwa na timu mbili, iliyobaki Dar kambini, na ile ya wachezaji waliokuwa wamekwenda kuzitumikia timu zao za taifa, ni kama timu mbili tofauti.

Tulipata muda mzuri wa kujumuika na kikosi cha timu ya vijana wa umri chini ya miaka 20, tulifanya nao mazoezi na tulicheza michezo miwili dhidi yao, hivyo wachezaji waliobaki kambini walipata muda wa kutengeneza pumzi na utimamu wa mwili, benchi la ufundi lilipata nafasi kuona wamefikia wapi na kutengeneza uwiano ili wenzao watakaorudi kutoka timu za taifa wake tayari," meneja huyo aliongeza.

Alisema Yanga haina hofu yoyote kue-


INAENDELEA UK. 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >